# Nipashe

Jumamosi Juni 3, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581330

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

## CCM wamvaa Msigwa lugha mikutano ya kisiasa

UKURASA 5



## Ummy atangaza Tanzania yaudhibiti ugonjwa Marburg

UKURASA 2



RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Kiini kifo mwanafunzi UDOM chawekwa wazi

UKURASA 3

UKURASA WA 7

## ZITTO ATAKA KUSAMEHEANA, APOKEA WANACHAMA WAPYA



KIONGOZI wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema watu wote walioachana katika mambo ya siasa kutokana na kila mmoja kuwa na chama chake, ni vyema kusameheana na kujenga...

UKURASA 17

## Rais Biden aanguka jukwaani



**Mapato yapaa, watalii wamiminika**





**Faru weusi, tembo waongezeka kwa kasi**

**Ndege mpya za doria kununuliwa**





**Moto Mlima Kilimanjaro waundiwa mkakati**

**Ajira mpya kutolewa, wahalifu 420 wanaswa**





Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24 bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwanga mpya Utalii

UKURASA 2

MICHEZO YANGA: TUMEFUATA KOMBE UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Ummy: Tanzania hakuna Marburg

**Na Titus Mwombeki,** KAGERA

SERIKALI imetangaza kusitishwa kwa mapambano dhidi ya ugonjwa wa Marburg mkoani Kagera baada ya kujiridhisha hakuna maambukizi mapya ya ugonjwa huo.

Ugonjwa wa Marburg uligundulika Machi 16 mwaka huu katika kata za Maruku na Kanyangareko wilayani Bukoba.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitangaza hali hiyo jana mkoani hapa wakati wa mkutano maalum uliohusisha wawakilishi kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF).

Waziri Ummy alisema watu wote waliohisiwa kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo waliokuwa chini ya uangalizi wa wataalamu wa afya wameruhusiwa baada ya kuridhiwa na matokeo ya vipimo vya mwisho vilivyofanyika ndani ya siku 42 tangu walipopokewa.

"Tangu kutangazwa kwa ugonjwa huo, watu tisa walibainika kuwa na maambukizi akiwamo mtoto, mtumishi mmoja wa afya na wengine wakiwa ni raia wa kawaida. Sita kati yao walifariki dunia akiwamo mtoto na mtumishi wa afya," alisema.

Waziri Ummy alisema wamefanikiwa kuudhibiti ugonjwa huo kwa muda mfupi pasi na madhara makubwa, hali iliyoipatia heshima Tanzania.

Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, alisema kati ya watu waliofuatiliwa walikuwa 212. Kati yao, 85 walikuwa watumishi wa afya, 117 walikuwa ndugu na jamaa wa wagonjwa waliogundulika, 15 walikuwa wanafunzi katika shule za sekondali waliokuwa wamelazwa katika hospitali ambazo wagonjwa wa mwanzo walifikishiwa.

"Kati ya hao 212 ni wawili tu ambao walionyesha dalili za ugonjwa huo na kuthibitika kuwa na ugonjwa wa Marburg. Kwa hiyo, taarifa ya mwanzo ilikuwa na wagonjwa saba baadaye kwa kuwafauatilia wagonjwa wawili waliongezeka na kufikia wagonjwa tisa," alisema Prof. Nagu.

Katibu Tawala Mkoa wa Kagera, Toba Nguvila aliwapongeza watu wote walioshiriki katika kupambana na ugonjwa huo hususani watumishi wa afya, mashirika ya kimataifa na wananchi wa kata za Maruku na Kanyangereko walioripoti kuhusu ugonjwa usiojulikana.



Katibu Mkuu wa Chama cha TLP, Richard Lyimo (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza maamuzi ya kikao cha kamati ya nidhamu ya chama hicho ya kumfukuza uanachama, Mwenyekiti wa Vijana wa chama hicho, Aivan Maganza kwa tuhuma za utovu wa nidhamu. Kulia ni Mwenyekiti wa Wanawake wa chama hicho Taifa, Nuru Kimwaga na Mjumbe wa Bodi ya wadhamini wa chama, Andason Temu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mwanga mpya Utalii

**Na Romana Mallya,** DODOMA

MWANGA mpya umeonekana katika utalii na uhifadhi nchini. Mapato ya utalii yameongezeka kukiwa na watalii milioni 3.454 mwaka 2022 kutoka milioni 1.711 mwaka 2021 huku idadi ya faru weusi nayo ikifikia 238 mwaka jana kutoka 163 mwaka 2019.

Hayo ni sehemu ya mafanikio makubwa 10 ya Wizara ya Maliasili na Utalii yaliyobainishwa jana bungeni jijini hapa na Waziri Mohamed Mchengerwa, alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Wizara hiyo imeliomba Bunge liidhinishe Sh. bilioni 654.668 kwa ajili ya mwaka huo wa fedha. Kati yake, Sh. bilioni 486.501 ni za matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 168.166 ni za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**WATALII WAMIMINIKA**

Waziri Mchengerwa alisema idadi ya watalii imeongezeka kutokana na juhudi mbalimbali zilizofanyika, ukiwamo uzinduzi wa Filamu ya Tanzania The Royal Tour aliyoshiriki Rais Samia Suluhu Hassan.

Alibainisha kuwa idadi ya watalii wa ndani na kimataifa waliotembelea maeneo ya hifadhi na Makumbusho ya Taifa imeongezeka kutoka watalii 1,711,625 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 3,818,180 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 123.

"Katika ongezeko hilo idadi ya watalii wa kimataifa imeongezeka kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 1,454,920 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 57.7.

Alisema idadi ya watalii wa ndani imeongezeka kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi 2,363,260 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 199.5. Wizara imeendelea kutangaza utalii kuyafikia masoko ya kimkakati yakiwamo ya Marekani, Ufaransa, Uingereza, Italia na China. Pia kupitia ligi kubwa za michezo za Marekani, Uingereza na Hispania.

"Mapato yatokanayo na watalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,310 mwaka 2021 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 2,527.72 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 93.

"Idadi ya watalii wa ndani katika robo ya kwanza ya mwaka 2023 imeongezeka hadi kufikia watalii 409,092, sawa na ongezeko la asilimia 41.4 kulinganishwa na watalii 289,372 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022," alisema.

**FARU WEUSI**

Waziri huyo alisema wameimarisha ulinzi wa rasilimali za wanyamapori na misitu na hivyo kuongezeka kwa idadi ya tembo kutoka 43,330 mwaka 2014 hadi 60,000 mwaka 2023 na kuifanya Tanzania kuendelea kuwa nchi ya tatu barani Afrika kwa faru weusi kuongezeka kutoka 163 mwaka 2019 hadi 238 mwaka 2022.

Alisema hiyo imesababisha wavuke lengo la Mkakati wa Kitaifa wa Kuhifadhi Faru 205 ifikapo Desemba 2023.

Mafanikio mengine aliyataja ni Tanzania kuendelea kuongoza duniani kwa kuwa na simba wengi wapatao 14,912 na twiga 24,000; kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2022 imekuwa nchi ya saba miongoni mwa nchi 18 za Afrika zilizo bora kutembelewa kiutalii.

Pia hifadhi tatu za Tanzania zimeingizwa katika orodha ya hifadhi 25 bora duniani kupitia Travelers' Choice Destination - National Parks of the World - Hifadhi ya Taifa Serengeti imekuwa ya kwanza ikifuatiwa na Hifadhi za Taifa Kilimanjaro (12) na Tarangire (14) kwa ripoti ya mwaka 2022.

Mchengerwa alitaja kufunguka kwa biashara ya hewa ya ukaa, kuimarika kwa maeneo ya Malikale na Makumbusho na kufanywa marekebisho ya Sheria ya Sekta ya Mambo ya Kale, Sura 333 ni sehemu ya mafanikio yao.

Waziri huyo aliitaja mikakati yao kwa mwaka ujao wa fedha ikijumuisha ununuzi wa ndege za doria za kukabiliana na majangili na vifaa maalum vya kukabiliana na majanga hifadhini, hasa moto Mlima Kilimanjaro.

Alisema mbali na ndege za doria, pia watanunua magari maalum, vifaa vya mawasiliano na vifaa vya kudhibiti moto. Alisema ndege mbili za doria zitakuwa mahususi kwa Hifadhi za Taifa Nyerere na Serengeti kwa ajili ya kudhibiti ujangili na wanyamapori wakali na waharibifu.

Pia alisema watajenga viwanja sita vya ndege katika Hifadhi za Taifa Ruaha (3), Mikumi (1) na Nyerere (2) na kukarabati viwanja 24 vya ndege katika Hifadhi za Taifa Nyerere, Serengeti, Katavi, Tarangire, Mto Ugalla na Burigi.

Waziri huyo pia alisema watafanya mapitio ya mipango ya ujumla ya usimamizi na uendelezaji wa Hifadhi za Taifa Tarangire, Saadani na Milima ya Udzungwa na kuchimba na kukarabati mabwawa sita kwa ajili ya matumizi ya wanyamapori katika Hifadhi za Taifa Mkomazi, Tarangire, Mikumi, Katavi, Ruaha,Saadani na Serengeti.

Pia aliitaja mikakati 10 kwa mwaka ujao wa fedha itakayofanyiwa kazi kukabiliana na changamoto za migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu na mipaka ya vijiji na hifadhi.

Alisema watatoa elimu na vifaa kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu, kutoa kifuta jasho na machozi kwa wanaoathirika na wanyamapori wakali na waharibifu, kufanya utafiti kwa kuwafunga mikanda ya mawasiliano viongozi wa makundi ya wanyamapori, kutumia ndege maalum kuondoa wanyamapori kwenye makazi, kuongeza vitendea kazi na askari wa kupambana nao. Pia kuunda kamati maalum ya wataalamu kumshauri. Kamati itaanza kazi mwezi ujao.

Waziri huyo pia alibainisha kuuawa kwa askari wanyamapori wa Jeshi la Uhifadhi wakiwa kazini. Wapo waliouawa kwa kuliwa na wanyamapori, kupigwa na majangili na wafugaji na wengine kujeruhiwa huku mmoja mpaka sasa akiwa hajulikani aliko.

Alisema wapo pia waliofariki dunia katika ajali ya maji wakati wakipambana na majangili na wengine katika matukio ya ndege zilizoanguka kwa nyakati tofauti wakitekelezaji majukumu yao ya kikazi.

Alisema wapo askari 13 wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) waliouawa na wananchi au majangili wa misitu katika maeneo mbalimbali.

Alisema watumishi 80 wataajiriwa kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika Pori la Akiba Pololeti; kununua magari kwa ajili ya utawala na kumalizia ujenzi wa Makao Makuu katika eneo la Kemyn katika Wilaya ya Karatu huku wahalifu 423 wa makosa mbalimbali wakikamatwa hifadhini.

HABARI KITAIFA

# Kiini kifo mwanafunzi UDOM chawekwa wazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UCHUNGUZI uliofanywa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), umebaini kifo cha mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Nusura Abdallah (pichani), hakina uhusiano wowote na ajali ya gari iliyomhusisha Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange.

Nusura alifariki dunia Mei Mosi katika Hospitali ya Faraja iliyoko Himo mkoani Kilimanjaro, huku mazingira ya kifo hicho yakizua utata baada ya watu kukihusisha na ajali ya Naibu Waziri huyo iliyotokea usiku wa kuamkia Aprili 26 mwaka huu. Kutokana na taharuki hiyo, THBUB iliamua kuchunguza.

Nusura alikuwa akisomea Shahada ya Kwanza ya Sanaa ya Elimu katika Ndaki ya Insia na Sayansi ya Jamii UDOM.

Mwenyekiti wa tume hiyo, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, akiwasilisha taarifa ya uchunguzi wa tukio hilo jana kwa waandishi wa habari jijini Dodoma, alisema hakuna uhusiano wowote baina ya kifo cha mwanafunzi huyo na ajali aliyopata Naibu Waziri Dugange.

"Mtakumbuka Mei 10, 2023, THBUB ilitoa taarifa kwa umma kupitia vyombo vya habari, ikielezea nia yake ya kufanya uchunguzi wa kifo cha aliyekuwa mwanafunzi wa UDOM, Nussura Hassan Abdallah, ambacho chanzo chake kilizua mkanganyiko. Baadhi ya watu walikihusisha na ajali ya gari iliyomhusu Dk. Festo Dugange, Naibu Waziri Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Afya)," alisema Jaji Mwaimu.

Alisema katika uchunguzi huo, THBUB ilitembelea eneo ilipotokea ajali ya gari iliyomhusisha Naibu Waziri Dugange, nyumbani kwake, kituo cha polisi (Trafiki) Mkoa wa Dodoma, Hospitali ya Benjamini Mkapa na UDOM.

Jaji Mwaimu alisema THBUB ilitembelea pia Kijiji cha Mandawa, Kata ya Mandawa Wilaya ya Singida Mjini wanakoishi wazazi wa marehemu, Kitongoji cha Mtakuja ulikozikwa mwili wa Nusura.

Alisema tume hiyo pia ilifika ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimnjaro, Hospitali ya Faraja iliyoko Himo na maeneo mengine kwa ajili ya kupata maelezo ya watu mbalimbali kuhusu mazingira ya kifo cha mwanafunzi huyo.

"Katika maeneo yote tume ilikokwenda ilipata ushirikiano wa hali ya juu kutoka kwa watu wote iliyowahitaji kupata maelezo yao," alisema.

Alifafanua kuwa baada ya uchunguzi, THBUB imebaini kuwa Mei Mosi, 2023, Nusura aliandaa chakula cha jioni ambacho alikula yeye, mchumba wake na mpwa wa mchumba wake.

Jaji Mwaimu alisema kuwa baada ya kumaliza kula, Nusura alijisikia vibaya na kuanza kutapika hadi kuishiwa nguvu, hali iliyosababisha kufikishwa Hospitali ya Faraja kwa matibabu.

Alisema kuwa pamoja na hatua mbalimbali za kitabibu zilizochukuliwa na madaktari wa hospitali hiyo,

Nusura alifariki dunia saa tano usiku wa Mei Mosi, 2023.

Pia alisema vipimo vilivyofanywa na hospitali hiyo vilionyesha kifo cha Nusura kilitokana na shambulio kali la kupanda kwa sukari na upungufu wa damu.

"Daktari aliyempatia huduma na ndugu wa marehemu waliotayarisha mwili kwa ajili ya mazishi na kuuona mwili huo kabla ya mazishi walithibitisha kuwa haukuwa na dalili za kupigwa, kujeruhiwa wala majeraha," alisema Jaji Mwaimu.



Pia alisema mabaki ya chakula walichokula Nusura, mchumba wake na mpwa wa mchumba wake na matapishi yaliwasilishwa katika Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa uchunguzi na baada ya kufanyiwa uchunguzi taarifa ilionyesha kutoonekana kwa dalili yoyote ya kuwamo sumu.

Alisema uchunguzi huo ulibaini pia gari lililopata ajali lilikuwa ni gari binafsi aina ya Toyota Land Cruiser GXR V8 lenye namba za usajili T454 DWV, lililokuwa linaendeshwa na Dk. Festo Dugange na alikuwa peke yake katika gari hilo.

"Kutokana na mazingira hayo, THBUB imebaini kuwa kifo cha Nusura hakikuwa na uhusiano wowote na ajali ya gari aina ya Toyota Land Cruiser GXR V8 lenye namba za usajili T454 DWV lililomhusisha Dk. Dugange, iliyotokea usiku wa Aprili 25 kuamkia 26 katika eneo la Iyumbu jijini Dodoma," alisema Jaji Mwaimu.

Alisema THBUB haikuweza kuthibitisha mtu yeyote kuhusika na kifo cha Nusura kutokana na vielelezo vya Hospitali ya Faraja, Mkemia Mkuu wa Serikali na maelezo ya mengine ya mashahidi. Vile vile, alisema tume hiyo inatambua hatua zinazoendelea kuchukuliwa na vyombo vingine likiwamo Jeshi la Polisi Tanzania na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (DPP) katika kulishughulikia suala hilo kijinai.

Alisema kutokana na uchunguzi wa vyombo hivyo, THBUB inapendekeza Jeshi la Polisi na mamlaka nyingine zichukuwe hatua ili kuwabaini wale wote wanaohusika na kutoa taarifa za uongo na chonganishi zinazosababisha taharuki katika jamii.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
02 . 06 . 2023

TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumatatu tarehe 05-06-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Rufiji, gari hizo zina namba za usajili:

**T 482 EAG / T 568 EAZ | T 118 EAG / T 877 EAU | T 460 DYG / T 879 EAU | T 973 DTN / T 572 EAZ**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 22.00 Upana - mita 5.00 Kimo - mita 4.70**

3. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti, gari zitasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**


## Kizimbani mashtaka ya kuua na kuondoka na nyeti za binadamu

**Na Rose Jacob,** MAGU

WATU watatu wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi wilayani Magu, wakikabiliwa na mashtaka ya mauaji ya Ester Lukonu (51) kisha kukata na kuondoka na nyeti zake hivi karibuni wilayani hapa.

Katika kesi hiyo ya jinai namba 6/2023, washtakiwa waliofikishwa mahakamani jana ni: Masunga Mabula (32), mkazi wa Nyanguge; Ezekiel Charles (45), mganga wa kienyeji na Mkazi wa Kisamba wilayani Magu; na Salome Raphael (32), mkazi wa Kisamba, Kata ya Lububu wilayani Magu.

Wote wanatuhumiwa na kuhusika na mauaji ya Ester Lukonu anayedaiwa kubakwa kisha kuuawa na watu hao ambao wanadaiwa kukata nyeti zake na kuondoka nazo kwa ajili ya imani za kishirikina.

Washtakiwa hao walipandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Magu, Amon Kahimba.

Hata hivyo, hakimu huyo hakuendelea kusikiliza kesi hiyo kutokana na Mahakama ya Hakimu Mkazi kutokuwa na uwezo wa kusikiliza kesi ya mauaji.

Baada ya washtakiwa kusomewa mashtaka yanayowakabili, Hakimu Kahimba aliiahirisha mpaka Juni 16 mwaka huu itakapohamishiwa Mahakama Kuu mkoani Mwanza kwa ajili ya watuhumiwa hao kusomewa maelezo ya awali.

Washtakiwa hao walikamatwa mwezi uliopita na Jeshi la Polisi mkoani Mwanza baada ya kutokea tukio la kuuawa kwa Ester na mabaki ya mwili wake kutelekezwa katika shamba la mihogo wilayani Magu.

Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Wilbroad Mutafungwa alifika katika eneo la tukio na kuahidi kutoa kitita cha fedha kwa atakayefanikisha kukamatwa kwa watuhumiwa. Siku chache baadaye watuhumiwa hao walikamatwa kunakodaiwa kwa mganga wa kienyeji kulikokuwa na nyeti za mwanamke zilizokaushwa kwa ajili ya mambo ya ushirikina.




# Serikali yaweka msimamo wa gharama kuunganisha umeme

**Na Romana Mallya,**
DODOMA

SERIKALI imesema inatamani suala la gharama za kuunganisha umeme kwa wananchi zipungue lakini kutokana na kuhitaji zaidi Sh. bilioni 156 kwa mwaka kufanikisha kazi hiyo, gharama hizo zinazotajwa kuwa kubwa zitaendelea kuwapo.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, aliyasema hayo juzi bungeni alipojibu baadhi ya hoja za wabunge waliochangia makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Byabato alisema wanatamani kupunguza gharama hizo kwa sasa lakini si rahisi na hawawezi kulifanya kwa haraka kwa sababu wanahitaji fedha zaidi.

"Gharama halisi za kuunganisha umeme ni wastani wa Sh. 700,000 kwa walio mita 30. Pale tunakounganisha umeme kwa Sh. 320,000 maana yake serikali imeweka ruzuku ya Sh. 380,000. Kwa wa vijijini wanaounganishwa kwa Sh. 27,000 imewekwa ruzuku Sh. 670,000. Gharama za sasa zina ruzuku kubwa.

"Januari mwaka jana, tulipofanya hesabu baada ya kurudi kwenye bei za zamani, TANESCO (Shirika la Umeme) ilibaini ongezeko la Sh. bilioni sita katika makusanyo ya gharama za kuunganisha.

"Kwa hiyo, kwa mwezi shirika linahitaji Sh. bilioni sita ili kuunganisha watu kwa gharama ya Sh. 27,000 wa mjini na linahitaji takribani Sh. bilioni saba kuunganisha wale wa vijijini.

"Kwa maana nyingine, tukitaka kuunganisha watanzania wote wanaohitaji umeme, tunahitaji takribani Sh. bilioni 13 ya ruzuku ili kuunganisha kwa Sh. 27000. Ukiipiga hii kwa mwaka ni Sh. bilioni 156.

"Jambo hili tunalielewa, tunatamani litokee, lakini sasa Sh. bilioni 156 inatoka wapi? Tunawaomba waheshimiwa wabunge, mturuhusu tuendelee kuchakata tuone namna ili fedha hii ya ruzuku ipatikane na gharama hizi ziweze kupunguzwa kwa wananchi," alisema.

Byabato alisema kwa sasa shughuli ya kubaini maeneo kwa uwezo wa wananchi na kiuchumi inaendelea na itakapokamilika, wataliunganisha na hilo ili wafikie sehemu ya kuunganisha umeme kwa gharama nafuu.

**BWAWA NYERERE**

Waziri wa Nishati, January Makamba, akijibu hoja kuhusu kuchelewa kukamilika kwa mradi wa uzalishaji umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, alisema Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ameweka wazi kwamba hakukuwa na ukadiriaji sahihi wa muda wa ujenzi, kitu ambacho ni kweli kwa kuwa hakuna mahali popote wanaweza kujenga megawati 2,115 kwa miaka mitatu.

Kuhusu muda kuongezeka alisema una namna ya kushughulikia hayo ndani ya mkataba ambapo hadi sasa hawajavunja kwa sababu ndani yake imeelezwa hiyo nyongeza itafanyikaje.

"Mradi unalelewa na uhusiano mzuri kati ya Tanzania na Misri, hauwezi kufeli, ndio maana hakuna mambo ya mahakamani. Katika mambo yanapaswa kutuunganisha ni mradi huu. Hii dhana kwamba wanataka kuhujumu, hawautaki, ninaomba huu mradi tusiutumie kupata sifa ya kisiasa.

"Kwamba mimi ndiyo mbabe zaidi ndiyo ninaweza kuusimamia kuliko wote waliopewa dhamana. Ninaomba siasa iwekwe pembeni, mradi huu ni mkubwa na wa heshima na fahari ya nchi yetu," alisema.

Waziri huyo pia alisema jamii ya Wahanzabe itapelekewa huduma ya umeme kabla ya mwezi Desemba mwaka huu, wakianza na umeme wa jua.

# Muliro ataja sababu polisi kuchelewa katika matukio

**Na Maulid Mmbaga**

KAMANDA wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, amesema taarifa za uhalifu zinatolewa na wananchi kwa wingi lakini wamekuwa wakichelewa kufika eneo la tukio kutokana na ugumu wa kufika eneo husika.

Akipokea msaada wa gari aina ya Toyota Hilux kutoka kwa Kampuni ya Motison Group,

Kamanda Muliro aliwaambia waandishi wa habari kuwa kutokana na changamoto hizo wanapopata wananchi wanaojua umuhimu wa usalama na kuwapatia vifaa hivyo, wanawasaidia kupata ufumbuzi wa upungufu huo.

"Mtu anakuambia kuna gari tunaliona Tegeta Nyuki linaendeshwa ovyo uelekeo wa Bagamoyo, likikamatwa inabidi ofisa aende pale kuchukua hatua za kisheria. Kwa hiyo, changamoto ya jinsi ya kufika haraka inakuwa ni miongoni mwa vinavyotukabili.

"Wananchi katika maeneo kama Kitunda, Mwanagati au Zingiziwa wanaweza wakakupa taarifa kuna jambo linataka kufanyika.

Sasa changamoto ya jinsi ya kufika eneo lile kwa haraka inakuwa ni kubwa na wakati mwingine unakuta wananchi wanalilaumu jeshi wanasema 'labda askari wanashirikiana na wahalifu, wanafika wamechelewa'," alisema.

Alisema Motison Group wameingia katika kusaidia vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi. Alishukuru kwa msaafa huo.

Mwakilishi wa Kampuni ya Motison Group, Pritesh Kuimji, akizungumza kwa niaba ya mkurugenzi wao, alisema wametoa msaada wa gari hilo baada ya kuridhika na kazi inayofanywa na Jeshi la Polisi na serikali kwa ujumla.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**MWALIKO WA MAFUNZO YA MATUMIZI YA MIFUMO YA KIELEKTRONIKI YA USIMAMIZI WA KODI YA ZUIO ILIYOBORESHWA (UPGRADED WITHHOLDING TAX MANAGEMENT SYSTEMS)**

**Dar es Salaam, 2 Juni, 2023:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango inapenda kuwajulisha walipakodi walio katika kundi la taasisi za umma nchini kuwa itafanya mafunzo maalum ya matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa kodi ya zuio (Withholding Tax) kufuatia maboresho yaliyofanyika hivi karibuni. Semina hii itafanyika siku ya J**umanne tarehe 6 Juni 2023** mkoani **Dodoma** katika Ukumbi wa **African Dream Hotel** kuanzia **Saa 3:00** asubuhi na itaendeshwa na TRA Makao Makuu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango.

Walipakodi walio katika kundi hili wanahimizwa kushiriki mafunzo haya ili kujijengea uwezo wa kuitumia mifumo hiyo kwa ufasaha na kuziwezesha taasisi kutimiza matakwa ya sheria na taratibu zinazosimamia utozaji wa kodi hiyo.

Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo karibu nawe au wasiliana nasi kupitia:

Tovuti : www.tra.go.tz
Piga simu bure : 0800-110016 au 0800-750 075 au 0800-780 078
WhatsApp : 0744 23 33 33
Barua Pepe : huduma@tra.go.tz

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na:

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

HABARI KITAIFA

# CCM wamvaa Msigwa lugha mikutano kisiasa

**Na Nebart Msokwa,** IRINGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimemjia juu aliyekuwa Mbunge wa Iringa Mjini (CHADEMA), Mch. Peter Msigwa, kikimtaka aache kutumia lugha mbaya dhidi ya viongozi.

Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) walipaza sauti zao dhidi ya Mch. Msigwa katika mkutano wa hadhara uliofanyika mjini Iringa wakati Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo alipohitimisha ziara yake ya siku sita mkoani hapa.

Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Musukuma, alimtaka Msigwa awaache viongozi wafanye kazi ya kuwaletea maendeleo wananchi badala ya kusimama majukwaani na kuwabeza.

Alidai Mch. Msigwa ni miongoni mwa viongozi wa vyama vya upinzani wanaotumia vibaya mikutano ya hadhara ambayo imeruhusiwa hivi karibuni baada ya kusitishwa kwa muda mrefu. Musukuma ambaye pia ni mjumbe wa NEC Taifa akiwakilisha Mkoa wa Geia, alirejea kauli yake aliyowahi kuisema bungeni ya kumtaka Mch. Msigwa alime nyanya badala ya siasa kwa madai kuwa hana uwezo wa kufanya siasa za kuleta maendeleo.

"Sisi hatutokuwa wapole kiasi hicho maana ninaona wenzetu wameanza kuutumia vibaya upole huu. Itakuwa ni jino kwa jino maana hata sisi tukishamaliza vikao vya Bunge tunarudi majimboni kupiga siasa. Mwambieni Msigwa akae kwa kutulia, mimi ni MNEC, niko huru kwenda kufanya siasa popote ndani ya nchi hii," alisema Musukuma.

Pia aliwataka madiwani na wabunge wanaotokana na CCM kuendelea kufanya kazi za kuleta maendeleo badala ya kukatishwa tamaa na viongozi wa vyama vya upinzani. Mbunge wa Mvumi mkoani Dodoma, Livingstone Lusinde, alisema kitendo cha Mch. Msigwa kutoa maneno makali dhidi ya viongozi wa CCM kinaharibu utaratibu wa maridhiano ulioanzishwa hivi karibuni, hivyo akamtaka aache.

Alisema Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na Rais Samia Suluhu Hassan ndiyo walioasisi maridhiano ambayo yalisaidia hata mikutano ya kisiasa kuruhusiwa na hivyo ni lazima maridhiano hayo yapewe heshima. Lusinde alisema CCM iko tayari kushirikiana na chama chochote ambacho kinataka kuwaletea wananchi maendeleo na hivyo akawataka viongozi wa CHADEMA kubadili mtazamo. Katibu Mkuu wa CCM, Chongolo, alisema serikali imesharidhia mchakato wa katiba mpya ambao ulikuwa umekwama kwa muda mrefu uendelee na hivyo akawataka watanzania kuwa watulivu wakati utaratibu unaendelea.

Alisema chama chake kinahitaji katiba mpya kuliko vyama vya upinzani na katiba inayohitajika ni ya watanzania wote na si kwa ajili ya kuwabeba wanasiasa peke yao.

Alisema viongozi wa CHADEMA wamekuwa wakiikosoa katiba iliyopo kwa kuangalia maslahi yao ya kisiasa badala ya kuangalia maslahi ya watanzania wote.

"Mchakato huo hauwezi ukaanzia pale ulipoishia. Wakati ule kuna mambo mengi sana yamebadilika. Sasa tusubiri timu iliyoundwa ilete maboresho, tunataka katiba mpya ambayo inawagusa mpaka wananchi wa kawaida," alisema Chongolo.

Aliwataka wananchi kuendelea kufanya kazi za kujiletea maendeleo na serikali itaendelea kuwawekea mazingira rafiki ya uzalishaji ili kuinua kipato cha mtanzania mmoja mmoja.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Mch. Msigwa ambaye ni Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, alifanya mkutano wa hadhara mjini Iringa na kutoa kauli mbalimbali dhidi ya viongozi wa CCM akiwamo Mjumbe wa NEC, Salim Abri (ASAS) na madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, akidai wameshindwa kuwaletea wananchi maendeleo.

# Kasi ya maambukizi VVU yapungua kwa 95%

**Na Mary Geofrey**

MGANGA Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, amesema kasi ya maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) imepungua kwa asilimia 95.

Pia amesema juhudi za kupunguza maambukizi hayo bado haziendani na Mpango wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

Prof. Nagu aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam alipotoa zawadi kwa wanafunzi bora wa kidato cha nne na sita wa masomo ya Kemia na Baiolojia zilizotolewa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA).

Alibainisha kuwa nchini kwa sasa watu milioni 1.7 wanaishi na VVU na kundi kubwa ni vijana. Aliwataka wahitimu wa sekondari nchini kuzingatia maadili kwa kuepuka tabia zisizofaa, kutunza afya na kujikinga na magonjwa ya zinaa na maambukizi ya VVU.

"Wanafunzi miliofanya vizuri kwenye masomo ya Kemia na Baiolojia mna wajibu wa kujitunza afya zenu ili kulisaidia taifa kubuni na kufanya uvumbuzi wenye tijam" alisema Prof. Nagu.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, alisema wametoa zawadi kwa wanafunzi 18 wa kidato cha nne na 18 wa kidato cha sita walioshika nafasi ya tatu bora kitaifa katika masomo ya Kemia na Baiologia.

Alisema pia wametoa zawadi kwa walimu wa masomo ya Kemia na Baiolojia ili kuongeza chachu ya kuendelea kubuni mbinu za ufundishaji na kufaulisha wanafunzi wengi zaidi.


## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kurudia minada ya hadhara kama ilivyohainishwa kwenye tangazo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| TEGETA | ITU COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 93457 KIWANJA NAMBA '1', KITALU 'G' MAPINGA ,KWA JINA LA ANDREW ANTHONY SINDABAHA. 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 89175 KIWANJA NA. '1157', KITALU 'A' TEGETA KWA JINA LA ANDREW ANTHONY SINDABAHA | ANDREW ANTHONY SINDABAHA | 1.MAPINGA BAGAMOYO 2.TEGETA | 20/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | OSCAR JOSSEY MUNIS | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | VERAELI ELIYA KOMBE | MWANANYAMALA -KINONDONI | 16/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HAPPYNESS GEORGE MKOPI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PATRICK SAMWEL NGAYIWA | KIJICHI MGENI NANI | 20/06/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | LILIAN FRANCIS MBETWA | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 100986,KIWANJA NAMBA 70 KITALU '18' | LEILA FRANCIS KAMA MLEZI WA AMIRI HAMISI IDDI | MAGOMENI | 09/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | MPOKI BROWN MWAIPASI | NYUMBA | MPOKI BROWN MWAIPASI | KILUVYA | 16/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ARUSHA | DAUSON LOIVOTI LAIZER | NYUMBA | DAUSON LOIVOTI LAIZER | OLKUNG'U-TERRAT ARUSHA | 19/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | EPHATA MICHAEL MOLLEL | NYUMBA | EPHATA MICHAEL MOLLEL | OLDADAI SOKONI II ARUSHA | 20/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | BEATRICE ALBERT OGAJA | NYUMBA | BEATRICE ALBERT OGAJA | ENGOSENGIU-ARUSHA | 21/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | BARAKAELI KUNDANDUNI MBISE | NYUMBA | BARAKAELI KUNDANDUNI MBISE | KINGORI-ARUSHA | 22/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | EMANUEL DANIEL SORORWA | NYUMBA | FRANK THOMAS KIVUYO | KITONGOJI CHA ILKIUSHIN KATA YA OLTURUMET ARUSHA | 20/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | HERIETH SENYAELY | NYUMBA | HERIETH SENYAELY | KING'ORI ARUSHA | 27/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | 1.NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.151,KITALU 'Q10' HATI NAMBA 143195-KIBAMBA 2.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO-CHAMAZI DOVYA | AHMAD KASSIM OMARY | 1.KIBAMBA 2.CHAMAZI DOVYA | 16/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.175184 KIWANJA NA.1370 KITALU "A" | KASSIAN ANTON NINDI | TABATA KISUKULU | 26/06/2023 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 22/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 20/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BRAITON RUBEN MWANKEMWA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | BRAITON RUBEN MWANKEMWA | IVUMWE -MBEYA | 16/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 15/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BARAKA PAUL DABAVUNJE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | BARAKA PAUL DABAVUNJE | UYOLE-MBEYA | 23/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 22/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 14/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | IGELEGELE BUGARIKA NA BUJINGWA-MWANZA | 20/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA | JAMES JACOB KALULEMA | MAHINA KANYERERE-MWANZA | 22/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | FELISTA MATOKE NYANGWE | NYUMBA YENYE HATI NA.45634,KIWANJA NA.183 KITALU 'B' | SOPHIA KIBOKO CHACHA | KISEKE-MWANZA | 16/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JUMANNE MOHAMED KAPOLI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MATHIAS CHARLES NDETTO | KISESA-MWANZA | 26/06/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 15/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 16/06/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JOSEPH KIGONGO IBAMBASI | NYUMBA | JOSEPH KIGONGO IBAMBASI | NYAKATO | 23/06/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| AGGREY | INNOCENT DIDAS MUMBURI | NYUMBA | KHADIJA SEIF SINKAMBA | VINGUNGUTI- ILALA | 20/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | JUTIA ABDALA SANZE | NYUMBA | JUTIA ABDALLA SANZE | PUGU BOMBANI -ILALA | 20/06/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| AGGREY | SAMSON MUSSA SAMANYI | NYUMBA | ZAKARIA WAMBURA NYAHULE | MAJOHE | 22/06/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | THOMAS REMI MARKUS | NYUMBA | THOMAS REMI MARKUS | TABATA KINYEREZI | 16/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | RAMADHANI HATIBU SAUKA | NYUMBA | JANE ELIAS MASALALILA | KITUNDA-ILALA | 22/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | GODFREY JOSEPH MZANJE | NYUMBA | GODFREY JOSEPH MZANJE | MARAMBA MAWILI | 23/06/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | DIANA MORRIS MSECHU | NYUMBA (2) | 1.MOHAMED HUSSEIN MBOWETO 2.DIANA MORRIS MSECHU | 1.MARAMBA MAWILI 2.MAJOHE | 23/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja,Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0715868000/0714939933/0754376493/0655715138/0765999000/0759648448
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga nafasi ya ubingwa wa CAF ipo, inawezekana

**INAWEZEKANA.** Ndio, wawakilishi wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Yanga ya Dar es Salaam bado wana nafasi ya kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

Fainali hizi huchezwa kwa dakika 180, tayari dakika 90 za awali zimeshachezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kwa wenyeji Yanga kukubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa wapinzani wao, watakapowakaribisha USM Alger kutoka Algeria.

Sasa leo Yanga itakuwa ugenini jijini Algiers kwa ajili ya kumaliza ngwe nyingine ya dakika 90 iliyobakia ili kukamilisha mechi hiyo ya fainali.

Na kama matokeo yatafanana, basi zitaongezwa dakika nyingine 30 au kufika hatua ya matuta, hadi mshindi wa fainali hiyo atakapopatikana.

Yanga inatarajiwa ifahamu kama USM Alger ilifanikiwa kupata ushindi hapa Dar es Salaam, basi wao pia wanaweza kupata ushindi wakiwa ugenini na kutimiza ndoto ambazo Tanzania inaziota kwa muda mrefu.

Ni ndoto ambayo kila mwanamichezo anapenda kuiona baada ya kuisubiri kwa muda mrefu, kwa sababu Tanzania imetuchukua miaka 30, kupata timu ambayo imefika fainali, mara ya mwisho ilikuwa mwaka 1993 na iliwakilishwa na Simba ambayo ilipoteza mchezo wa marudiano tena ikiwa nyumbani. Hayo yalipita, sasa hivi ni wawakilishi wetu kabla ya kufika hatua hii, wamekutana na changamoto mbalimbali, wachezaji wake wameiva na wamejipanga kuweka historia.

Wachezaji wa Yanga wanatakiwa wakumbuke sasa wanapeperusha bendera ya Watanzania na si ya klabu yao pekee, wanatakiwa washuke dimbani wakifahamu nchi inawaombea mafanikio katika mechi hiyo ya marudiano. Hatua ambayo Yanga imefikia bado ni ya kuwapongeza, kufungwa katika mechi ya kwanza isiwe chanzo cha kuwakatisha tamaa wachezaji, hapana, kwa kawaida fainali bado haijamalizika.

Wachezaji wa Yanga wanatakiwa wafahamu mbali na kubeba bendera ya Tanzania na klabu yao, wafahamu wazi watakapofanikiwa kuibuka mabingwa wa mashindano hayo ambayo ni ya pili kwa ukubwa katika ngazi ya klabu yanayoandaliwa kila mwaka na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kutawaongezea thamani, hivyo waingie dimbani kwa kuonyesha viwango vya juu. Fainali hizi si zitawapata heshima, lakini wafahamu kutwaa ubingwa kutawafungulia fursa mbalimbali za kwenda kucheza katika klabu nyingine kubwa za ndani na nje ya Afrika na hata mataifa ya Ulaya.

Zawadi ya ubingwa watakayopata kutoka CAF, itawasaidia katika kutimiza mahitaji binafsi mbalimbali ambayo kama wafanyakazi wengine wanafikiria kuyatekeleza katika ndoto zao za kila siku, na tayari bosi wa klabu ameshaweka wazi kiasi cha asilimia 40 kitagawiwa kwa wachezaji.

Katika kuonyesha nchi iko pamoja na mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa 2022/2023, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, alitoa ndege ambayo ilisafirisha msafara wa timu hiyo ili kuwarahisishia njia ya kufika kwenye kituo cha fainali kwa wepesi, hilo ni deni, hivyo wachezaji wa Yanga mnatakiwa kupambana na hatimaye kumpa mama furaha.

Kama haitoshi, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, juzi bungeni ameweka wazi bado anaamini Yanga ina nafasi ya kuweka historia kwa kutwaa ubingwa wa mashindano hayo, wachezaji msikate tamaa, kuweni makini kwa kila nafasi ambayo mtaipata, taifa linawaombea dua njema.


Nipashe inawatakia kila la heri wachezaji wa Yanga katika kuhakikisha mnaonyesha kandanda safi na kusaka ushindi, lakini mkicheza kwa nidhamu wakati wote. Tunawakumbusha hakuna fainali rahisi, USM Alger pia inafahamu licha ya kupata ushindi ugenini, inahitaji kupambana kulinda ushindi wake, hivyo kucheza kwa tahadhari ni muhimu, kila mmoja anatakiwa kuhakikisha anafanya vyema majukumu yake.

Nyota njema ya Yanga katika mashindano ya kimataifa msimu huu ilianza kuonekana mapema, katika mechi ya mtoano ambayo walimalizia ugenini dhidi ya Club Africain ya Tunisia, ilionekana wanaenda kukamilisha ratiba lakini iliwaondoa Waarabu hao, pia ilipata matokeo mazuri katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya ugenini, hivyo leo kwa mara nyingine na mara ya kwanza mnaweza kushinda ugenini na kutwaa ubingwa.

Kila la heri Yanga, Mungu ibariki Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kila la heri Yanga kwa heshima mliyoipa nchi

Na Adam Fungamwango

**WAWAKILISHI** wa Tanzania katika michuano ya Kombe la Shirikisho, Yanga leo saa 4:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki, watakuwa kwenye dimba la Juillet wa Tano jijini, Algiers nchini Algeria kucheza dhidi ya wenyeji, Union Sportive de la Medina d'Alger kwa kifupi USMA.

Ni mechi ya fainali ya pili baada ya ile iliyochezwa nchini Jumapili iliyopita, wageni wakishinda mabao 2-1, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ukivuta kumbukumbu nyuma wakati Yanga inaanza michuano ya kimataifa, hasa ilivyoanza Ligi ya Mabingwa Afrika, haikutarajiwa kabisa kama inaweza kufika hapa.

Ilitoa sare ya bao 1-1 dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan, na kwenda kupoteza goli 1-0 ugenini. Hakukuwa na matumaini yoyote ya Yanga kutinga hata kwenye hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.

Ilipotupwa kwenye mechi za 'play off', ilipangiwa kucheza dhidi ya Club Africain ya Tunisia, moja ya klabu bora na tishio Afrika.

Mechi ya kwanza ilikuwa suluhu, huku matumaini ya kusonga mbele hatua ya makundi yalififia.

Katika hali isiyotarajiwa, Yanga ilishinda bao 1-0 ugenini na kutinga hatua hiyo kwa kishindo. Lengo la viongozi wa Yanga sasa lilibadilika, badala ya kutinga makundi, sasa lilikuwa ni kuvuka hatua hiyo tu.

Safari ya ajabu ya Yanga iliendelea, wakati mashabiki wengi wa soka wakiona kama inashiriki tu michuano hiyo, huku kumbukumbu zikionyesha ilishawahi kucheza hatua za makundi Kombe la Shirikisho, mwaka 2016 na 2018, wakishika mkia kwenye hatua hiyo, hawakutarajia sana makubwa.

Hata hivyo, Yanga iliendelea kushangaza wengi kwa matokeo iliyokuwa inayapata kwenye michuano hiyo, hasa ugenini ambapo ilicheza mechi sita kutoka 'play off' hadi fainali na ikashinda ugenini mechi nne.

Haikushinda kwenye mechi mbili tu, dhidi ya US Monastir ya Tunisia ilipofungwa mabao 2-0 na sare ya bao 1-1 dhidi ya Real Bamako ya Mali.

Katika hali ambayo haikutarajiwa, Yanga ilimaliza ikiliongoza Kundi D, ikiwa na pointi 13, ikishinda mechi nne, sare moja na kupoteza moja, mbele ya timu kongwe na zenye uzoefu katika michuano hiyo kama TP Mazembe.

Na kwa mara ya kwanza ikaifunga TP Mazembe, nyumbani na ugenini, ikiweka rekodi ya kuwa timu ya kwanza Bongo kufanya hivyo.

Kwa takwimu na rekodi hizo ambazo Yanga imeweka, ni sababu tosha ya mashabiki wengi bado kuwa na matumaini makubwa ya kufanya vizuri kwenye mechi ya marudiano. Ni kwa sababu rekodi zinawabeba ikicheza ugenini.

Kuna rekodi itawekwa ya straika Fiston Mayele kutwaa kiatu cha dhahabu, ambapo itakuwa kwa mara ya kwanza klabu ya Tanzania kutoa mfungaji bora kwenye michuano hiyo.

Mayele ana mabao saba huku akiwapita Khaled Bousseliou mwenye magoli manne na Zinneddine Belaid aliyefunga matatu, wote wa USM Alger.Ugumu wa mechi hiyo ya fainali inawafanya kuwa vigumu sana kumfikia.

Matokeo yoyote yatakayotokea, hata kama Yanga ikipoteza, bado watahesabiliwa kama mashujaa wa nchi, kwa sababu msimu huu wamefanya kitu ambacho hakikutarajiwa, 'sapraizi' za mashabiki wote wa soka Afrika.

Kufika fainali kwa timu ambayo haikutarajiwa hata kuingia makundi ni ushindi mkubwa na inastahili kupongezwa, sidhani kama itatokea kuukosa ubingwa akaanza kutafutwa mchawi wa kubebeshwa lawama.

Kiwango na mahali ilipofikia Yanga ni heshima kwao na soka la Tanzania ambayo ligi yake inatajwa kuwa ni ya tano kwa ubora baada ya ligi ya Misri, Algeria, Morocco na Sudan.

Kuna baadhi ya wadau wa soka walikuwa hawakubaliani na hili, lakini msimu huu tu baada ya Yanga na Simba kunyanyasa kwenye michuano ya kimataifa, nadhani sasa wameanza kuamini.

Matumaini yangu hali hii iendelee kila mwaka na isiwe kama wamebahatisha. Naitakia kila la kheri Yanga kwenye mechi ya leo, na matokeo yoyote yatakayopatikana bado ni washindi tu.

## HABARI KITAIFA

# Zitto ataka kusameheana, apokea wanachama wapya

**Na Julieth Mkireri,** KIGOMA

KIONGOZI wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema watu wote walioachana katika mambo ya siasa kutokana na kila mmoja kuwa na chama chake, ni vyema kusameheana na kujenga chama kwa kuwatetea wananchi na wakazi wa Mkoa wa Kigoma.

Zitto alitoa kauli hiyo jana katika mkutano wa kumkaribisha mwanasiasa Kiza Mayeye ambaye hivi karibuni alijiunga na chama hicho akitokea Chama cha Wananchi (CUF).

"Ninawaomba watu wote ambao tuliachiana njia, tuwiane radhi, sote kwa pamoja tuwe pamoja, iwe ni vigumu kutugombanisha. Binafsi ninaomba radhi. Hata kama hatujaombana radhi, turudini wote katika chombo kimoja sasa," alisema Zitto.

Alisema kuwa katika mambo ya kisiasa, kuna mambo mengi na hivyo kuomba walioachana awali, kujiunga sasa na kuwa kitu kimoja kukijenga chama chao na kuwatetea wananchi katika masuala ya maendeleo.

Zitto alisema Kiza yupo katika jukwaa sahihi na watafanya kazi pamoja kwa kusaidiana kuhakikisha wanasukuma mbele sauti ya wana Kigoma Kaskazini.

"Kiza alinifuata akaniambia amefuatwa na vyama tofauti lakini yeye ameamua kufanya kazi na ACT Wazelendo, nikaona ni jambo la busara alilolifanya, amechagua chama kinachokwenda kuwatetea wananchi wa Kigoma na maeneo mengine nchini.

Zitto aliwataka wakazi wa Mkoa wa Kigoma kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha majimbo yote ya Kigoma yanaongozwa na viongozi wa ACT Wazalendo.

Kiza aliwashukuru viongozi wa ACT Wazalendo kwa kuamua kukubali kufanya naye kazi, akisitiza katika siasa hakuna adui wa kudumu wala rafiki wa kudumu.

Katika mkutano huo, aliyekuwa Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kigoma, Kalembe Masud na mwanachama mwingine, Lumu Hamis, walijiunga na ACT Wazalendo.

# Kampuni kunufaika fursa nishati safi EU

**Na John Badi**

KAMPUNI zilizopo ndani ya mnyororo wa thamani wa nishati safi za kupikia zitakuwa na fursa za kupanua biashara kupitia programu inayodhaminiwa na Mfuko wa Umoja wa Ulaya (EU) katika mikoa ya Pwani, Morogoro, Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma.

Mfuko huo upo chini ya programu ya mbinu jumuishi kuelekea suluhisho endelevu ya nishati safi ya kupikia na Mfuko Maendeleo wa 11 wa Ulaya (EDF). UNCDF ni mtekelezaji mkuu na msimamizi wa mfuko wa programu hiyo inayotekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na UNIDO.

UNIDO inalenga kupanua matumizi ya bioethanol kwa Mkoa wa Dar es Salaam pekee. Kama washirika wa utekelezaji, UNCDF inahamasisha ongezeko la soko la nishati safi ya kupikia kwa ajili ya kupambana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na ukataji miti na upikaji unaoleta athari.

Mkuu wa UNCDF, Peter Malika, alisema juzi "...kupitia programu hii ya Cookfund, tunalenga kukuza maendelo ya soko la nishati safi za kupikia huku tukiangazia kuhakikisha upatikanaji na unafuu kwa mtumiaji na mwendelezo wa masoko.

"Wito wa pili kwa washiriki utakwenda hadi tarehe 30 Septemba 2023 ambapo ruzuku ya zaidi Sh. bilioni 10 za kitanzania iko tayari kwa ajili ya kupanua uzalishaji na usambazaji wa nishati safi za kupikia kwa biashara zitakazokidhi vigezo ili kutoa mbadala ulio rafiki kwa mazingira dhidi ya mbinu za mapishi zilizozoeleka kitamaduni.

"UNCDF Tanzania, kama mshirika wa utekelezaji, itasimamia mchakato wa uchaguzi na utoaji wa fedha kwa kampuni zilizofanikiwa pamoja na maendeleo ya huduma za biashara zinazotakiwa."

# DAWASA yazisogeza huduma kwa wananchi

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) imeendelea kuwafikia wananchi wengi zaidi kwa kuwasogezea huduma kupitia madawati ya huduma kwa wateja yaliyofunguliwa maeneo mbalimbali.

Kupitia mkoa wa kihuduma DAWASA Mivumoni, jumla ya madawati manne yamefunguliwa katika mitaa ya Wazo, Kulangwa, Mivumomi CCM na Muungano ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanafikiwa na kupatiwa huduma ya majisafi.

Ofisa Huduma kwa Wateja DAWASA Mivumoni, Neema Arthur, alisema kuwapo madawati ya huduma kwa wateja kumeisaidia mamlaka kuwafikia wananchi wengi kwa wakati mmoja na kuongeza idadi ya wateja kwa kiasi kikubwa.

"Wananchi wengi wamejitokeza kupata huduma kupitia madawati haya, hii imetusaidia kuongeza wateja lakini zaidi kuwapatia wananchi huduma ya majisafi kwa haraka," alisema Neema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kulangwa, Husna Yasin, alisisitiza wananchi kuendelea kujitokeza kwa wingi kwa kuwa hiyo ni nafasi nzuri waliyoihitaji wapate huduma ya majisafi.


# NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED** na **STEAM GENERATION RECOVERIES LTD**, Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | GODWIN MAGAYANE KAMBUGA | GODWIN MAGAYANE KAMBUGA | GARI YENYE USAJILI No. T 286 DCP CIVIC HONDA | AFRICANA, KATA YA MBEZI, WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM. | 17/06/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | STEAM GENERATION RECOVERIES LTD |
| 2 | DEOGRATIUS JOHN MALYA | DEOGRATIUS MALYA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA | BOMA NG'OMBE KATA YA KAMBI YA RAHA WILAYA YA MOSHI MJINI | 17/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 3 | SPRIAN GEORGE CHUWA | SPYRIAN GEORGE CHUWA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA | JITENGENI KATA YA MJI MPYA WILAYA YA MOSHI | 19/06/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 4 | YONA MARTIN MJEMA | YONA M. MJEMA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA | KILEO KATA YA KILEO MWANGA WILAYA YA MWANGA | 20/06/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 5 | WINFRIDA J. MUSHI | WINFRIDA J. MUSHI | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA | MSUFINI, KATA YA MSARANGA , WILAYA YA MOSHI MJINI | 19/06/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 6 | SETH ERNEST ZAKARIA | SETH ERNEST ZAKARIA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA | MTAA WA VIWEGE , KATA YA MAJOHE , WILAYA YA ILALA | 19/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 7 | ALEDONGI COMPANY | RAHEL E. MTAYOBA | KIWANJA CHENYE LESENI NAMBA DSMT1010635 | SALASALA , WILAYA YA KINONDONI-DAR ES SALAAM | 21/06/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 8 | COSMAS B. MUSHI | SCOLASTICA G. MUSHI | KIWANJA CHENYE HATI YA MAUZIANO NO P.LH.9A S/MTAA | MTAA WA MSUMI KATA YA MBEZI WILAYA YA UBUNGO | 22/06/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 9 | FROLA MKWAY | FLORA MKWAY | KIWANJA CHENYE HATI YA MAUZIANO S/MTAA | MTAA WA UWANJA WA NDEGE KATA YA KIPAWA WILAYA YA ILALA | 20/06/2023 SAA 06:00 MCHANA NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED**
**P. O. Box 62163**
**Dar es Salaam**
**Tel: 0658100737, 0757276263**
**Email: amazauctionma@gmail.com**

**STEAM GENERATION RECOVERIES LTD**
**P.O. Box 80607**
**Dar es Salaam**
**Tel: 0674588876, 0715917451**
**Email: steam@steamtz.com**

HABARI KITAIFA

# Watafiti watoa mbegu nane za muhogo Lindi na Mtwara

**Na Hamisi Nasri,** LINDI

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI) imewataka wakulima wa muhogo katika mikoa ya Lindi na Mtwara kuongeza uzalishaji ili kukuza kipato na kukabiliana na uhaba wa chakula kwa familia.

Akizungumza na wakulima, Mtafiti wa Mazao Jamii ya Mizizi ya Viazi na Mihogo kutoka TARI Naliendele, Festo Masisila, alisema wametoa mbegu nane na kuziweka katika shamba moja la kata ili kuwezesha wakulima kujifunza kwa vitendo.

Mtafiti huyo alisema shamba hilo lilikuwa na mbegu bora aina nane ambazo kati yake, zimo za Taricas 1,2,3,4,5, mkumba, chereko, mkuranga kiroba na kipusa ambazo zimedhibitishwa na Tosc tangu mwaka 2009.

Alisema mbegu hizo zinafaa, pia zinavumilia magonjwa ikiwamo batobato kali pamoja na michirizi kahawia, ndio maana waliweka shamba darasa ili wakulima wawe na machaguo kulingana na sifa mbalimbali zitakazowafaa katika eneo lao.

Mtafiti Msaidizi kutoka TARI Naliendele, Dwasi Gambo alisema wanavuna mihogo waliyoipanda katika shamba darasa la Kata ya Mangopachanne, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara ambako wakulima walishirikishwa katika hatua zote.

"Leo tunavuna mbegu kwa kujumuisha wakulima katika shamba darasa lenye mbegu aina tisa ili kuwafanya wakulima watambue na kuzifahamu mbegu zote na kuona ipi ni bora kwao," alisema.

Benita Mkanga, mkulima wa Kijiji cha Maumbika mkoani Lindi, alisema amekuwa akitumia mbegu za kienyeji kwa miaka mingi bila kuona tija katika kilimo chake cha muhogo. Upatikanaji wa mbegu bora unampa nguvu ya kuendelea kulima.

"Nimetumia mbegu za kienyeji kwa muda mrefu ambazo hazikuwa na tija kwangu, Ninaamini kuwa nikitoka katika shamba darasa, ninakwenda kuwa na kilimo bora kwa sababu ninaamini kuwa mbegu hii imenitoa katika sehemu moja na kuniweka katika sehemu nyingine," alitamba.

Abdulahman Ekapu, mkazi wa Kijiji cha Mangopachanne mkoani Mtwara, alisema kuwa zao hilo ni tegemeo kwake kwa kuwa amekuwa akilima kwa ajili ya biashara na chakula nyumbani.

Alisema elimu hiyo ya utafiti shirikishi ni elimu bora ambayo serikali imeona inafaa kwa kuwa sio tu inafanywa kwa vitendo, bali wakulima wanafanya wenyewe kwa maelekezo ya watalaamu.

Ofisa Kilimo Kata ya Mangopacha, Irene Ngowi, alisema kupitia shamba darasa hilo wakulima wamejifunza mambo mengi kuanzia kuandaa shamba hadi kuvuna, hali ambayo itawabadilisha na kuwafanya waanze kulima kisasa zaidi.

"Wakulima wamejifunza na wameona mbegu gani nzuri zinawafaa kwa chakula na biashara.

Ni vyema watafiti wakaweka mikakati ya kutuletea mbegu inayofaa kwa wingi na kwa wakati hata kama ni kwa gharama nafuu tununue," alisema Irene.




Ofisa Miradi kwa CRS TZ, Emmanuel Akyoo akitoa mada kuhusu umuhimu wa mawasiliano na michezo kwa watoto, alipokutana na wazazi na walezi wa watoto waliopona na wale wanaoendelea na matibabu ya mguu kifundo katika Hospitali ya CCBRT, Dar es Salaam jana, wakati wa kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Miguu Kifundo ambayo huadhimishwa Juni 3 kila mwaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC ataka uwekezaji zaidi katika mkonge

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima amewataka viongozi na watendaji wa ngazi za mkoa na wilaya kuongeza nguvu katika uwekezaji wa zao la mkonge ambalo kwa sasa lina soko kubwa kimataifa.

Amesema bidhaa za zao hilo huoza kwa urahisi na hivyo ni muhimu katika utunzaji wa mazingira kulinganishwa na bidhaa za plastiki.

Malima aliagiza hayo mjini Morogoro wakati wa makabidhiano ya ofisi na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo, Fatma Mwasa ambaye kwa sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Kagera.

Alisema kuwa awali mkonge ulikuwa unachangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa Mkoa wa Morogoro, hasa miaka ya 1960 lakini kwa sasa zao hilo limerudi nyuma kwa zaidi ya asilimia 80.

"Wakati Tanzania ilikuwa mzalishaji mkuu wa mkonge dunia nzima miaka 1963 hadi 1968, Morogoro ilikuwa inazalisha tani 250,000 za mkonge na wakati matumizi ya zao la mkonge duniani yalipobadilishwa na kuwa bidhaa za pastiki, sisi tukasinzia tukajikuta tunatoka katika kuzalisha tani 250,000 hadi sasa 16,000," alieleza.

Malima alisema dunia kwa sasa imegundua umuhimu wa kutumia bidhaa zinazoweza kuoza hivyo kurejesha matumizi ya bidhaa zinazotokana na mkonge.

"Ni muhimu sasa Morogoro tukaongeza uzalishaji kutokana na umuhimu wa zao hili. Katika Ilani ya CCM, nchi inatakiwa kuongeza mkonge kufikia tani 1,500,000 ifikapo kwa mwaka 2025, lakini sisi tumekusudia kufikia tani milioni moja," alisema.

Mkuu wa Mkoa aliwataka viongozi na watendaji kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji ili mifugo itumike kama rasilimali za kiuchumi badala ya kugeuka wadudu wanaoleta migogoro.

"Morogoro ina mambo mazuri, ina sifa nzuri tangu zamani ikiwamo katika uwekezaji wa kilimo. Haiwezi kutambulika kwa sifa mbaya ya migogoro ya ardhi badala ya mambo mazuri yaliyopo," alionya.

Aliwataka wafugaji kufuga kwa tija ili mifugo yao iwe rasilimali ya kukuza uchumi na wakulima kujipanga kwa uwekezaji mkubwa kutokana na wawekezaji kuonyesha nia ya kuwekeza zaidi katika kilimo, hasa cha miwa.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatma Mwasa alisema Mkoa wa Morogoro una changamoto kubwa ya migogoro ya wakulima na wafugaji inayotokana na wageni kukaribishwa na baadaye kuchukua maeneo makubwa, kisha kutaka kuwaondoa waliowakuta.

# Wadau wateta mpango wa kutokomeza malaria

**Na Halfani Chusi**

KATIKA kuhakikisha mpango wa serikali wa kutomeza malaria mpaka ifikapo 2030 unafanikiwa, Taasisi ya Afya ya Ifakara (IHI) kupitia watafiti wake kwa kushirikiana na serikali, wamekutana kwa ajili ya mjadala wa pamoja kuangalia namna ya kufikia lengo hilo.

Mkutano huo ulifanyika jana jijini Dar es Salaam, ukiwakutanisha wadau mbalimbali wa Sekta ya Afya kujadili na kutoka na jibu la pamoja litakalokuwa na mikakati kabambe ya kutomeza malaria kufikia vifo sifuri. Kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, Mkurugenzi wa Afya ya Uzazi Mama na Mtoto, Ahmad Makuwani, alisema ushauri utakaotolewa na watafiti hao, watauchukua na kwenda kuufanyia kazi ili kutomeza malaria.

Alisema lengo la serikali ni kutokomeza, siyo kudhibiti. Imepanga kupokea ushauri kutoka kwa wataalamu mbalimbali na kuutumia ili kufikia adhima ya vifo sifuri vitokanavyo na ugonjwa huo.

"Tupo katika majadiliano ya pamoja na Watafiti kutoka IHI, tunajadili mafanikio na changamoto katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria na baadaye serikali tutaubeba ushauri wao kwa sababu wao ni watafiti, tutakwenda kuutumia ili kutokomeza malaria," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Afya Ifakara, Honarati Masanja, alisema mpango huo ulianza muda mrefu, lakini ulikwama kutokana na masuala ya kifedha, akisistiza lengo lao ni kuhakikisha wanatokomeza malaria kama walivyofanikiwa kwa Tanzania Zanzibar.

Alisema majukwaa kama hayo yanatoa fursa kwa wadau kukusanyika pamoja na kujadili njia mbalimbali za kutokomeza malaria, hata kuangalia ile mikoa ambayo maambukizi yapo juu kwa kutoa elimu ya afua.

"Ukiangalia kuna mikoa kama Katavi na Kagera inatajwa kuwa na maambukizi mengi ya malaria. Kwa hiyo, tutaanzia huko kwa kutoa afua na elimu kwa sababu majukwaa haya pia yanatupa nafasi ya kuangalia wapi tulipo na tunapokwenda," alisema.

Msaidizi wa Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar, Safia Mohamed Ali alisema wamefanikiwa kutokomeza ugonjwa huo kutokana na idadi ndogo ya watu na ugawaji wa afua bila upendeleo.

Alikumbusha kuwa mwaka 1969 Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitangaza Zanzibar kuwa imefanikiwa kutokomeza malaria, jambo ambalo liliwafanya waendelee kuweka misingi imara na thabiti, ikiwamo kutoa elimu ya usafi wa mazingira na kugawa vyandarua kwa wajawazito na wenye watoto wadogo. Mbunge wa Nzega Vijijini, Dk. Hamisi Kigwangalla, alisema kazi ya Bunge ni kuishauri serikali na ataufikisha bungeni ushauri wa wataalamu hao ili serikali iutumie katika kampeni hiyo.

Mjumbe wa Mpango wa Kuzuia Maralia nchini, Zuwena Mohamed, maarufu Shilole, alisema atatumia nafasi aliyonayo katika jamii kutoa elimu ya kutokomeza mazalia ya mbu ambayo ndio chanzo cha ugonjwa huo.



# ‘Fikisheni huduma ya maji maeneo muhimu ya kijamii’

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MAMLAKA za maji nchini zimetakiwa kuhakikisha zinaweka kipaumbele cha kufikisha huduma ya maji katika maeneo ya muhimu ya kijamii kwenye mikoa yao.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprica Mahundi alitoa agizo hilo wakati wa kuzindua mradi wa maji eneo la Chimalaa Ntyuka jijini hapa juzi.

Mahundi, alizitaka mamlaka hizo za maji nchini kuhakikisha kuwa wanatoa kipaumbele cha kufikisha huduma ya maji kwenye maeneo yenye huduma za kijamii.

“Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha nyingi kwenye miradi ya maji kwa lengo la kuhakikisha wananchi wengi wanafikiwa na huduma hii ya maji,”alisema

Kahdalika alisema maeneo hayo ya kutoa huduma za kijamii ni sehemu mhimu ambayo inatakiwa kufikishiwa huduma ya maji kutokana na kutumiwa na watu wengi.

Alitayaja maeneo hayo yanayotakiwa kufikishiwa huduma ya maji kuwa ni hospitali, zahanati, vituo vya afya, shule Mahakama na vyuo mbalimbali.

Alibanisha kuwa amekuwa akipata malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu baadhi ya maeneo hayo hasa yaliyopo vijijini kutofikishiwa huduma hiyo.

Wakati huo huo, alizindua bodi ya tisa ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA).

Katika uzinduzi huo aliitaka bodi mpya kuhakikisha inaendeleza yale mazuri yaliyofanywa na uongozi uliopita pamoja na kuongeza ubunifu ili kuisaidia mamlaka hiyo kuendelea kufanya vizuri kwahudumia wananchi.

Awali akitoa taarifa ya mradi huo Mkurungenzi wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph alisema walipokea Sh.bilioni 3.5 kutoka serikalini kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

Mhandisi Joseph alisema fedha hizo hazikutosha kukamilisha mradi huo mpaka kufikisha maji kwa wananchi kwa awamu ya kwanza, hivyo DUWASA kupitia makusanyo yake ya ndani iliongeza Sh. milioni 112 kugharamia baadhi ya kazi ili kukamilisha mradi.

Mkurungenzi huyo alisema gharama zote za kutekeleza mradi kwa awamu ya kwanza kiasi zilizotumika ni Sh. milioni 471.8.

Aliongeza kuwa katika kukabiliana na athari za ugonjwa wa UVIKO-19, serikali ilitenga Sh. bilioni 1.1 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji safi.

Alisema eneo la Ntyuka Chimalaa lilitengewa Sh.milioni 359.7, Bahi Sh.milioni 451.6 pamoja na uchimbaji na ukarabati wa visima Sh. milioni 289.7 kwa maeneo ya pembezoni mwa Mkoa wa Dodoma.

Alisema mradi wa Ntyuka Chimalaa uligawanywa katika awamu mbili kulingana na upatikanaji wa fedha; ambapo awamu ya kwanza ilikuwa uchimbaji wa visima, ujenzi wa vibanda vya kuendeshea pampu, usimikaji wa pampu na ujenzi wa tenki.

Mradi huo ulitekelezwa na kukamilika kwa miezi sita, ulianza Januari mosi 2022 na ulikamilika Juni 30, mwaka huu na lengo la mradi huo ni kuboresha hali ya upatikanaji maji kutoka asilimia 0 mpaka 95, utawanufaisha wakazi 4,441.

# Mawakili 600 kupewa mafunzo ya kuongeza ufanisi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAWAKILI wa serikali zaidi ya 600 wanatarajia kupata mafunzo ya kujengea uwezo katika masuala mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika utelezaji wa majukumu yao ya kila siku kwa weledi mkubwa.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Boniphace Luhende, alisema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya miaka mitano tangu kuanzishwa kwa ofisi hiyo mwaka 2018.

Alisema maadhimisho hayo yatafanyika jijini hapa, Juni 5, mwaka huu na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Dk. Luhende, alisema mawakili wa serikali watakaopewa mafunzo hayo ni kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wizara zote, idara, taasisi za serikali, mikoa pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

“Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imealika wakufunzi wabobezi 24, ambao ni majaji na majaji wastaafu kutoka Mahakama Kuu ya Tanzania, Mahakama ya Rufani, wataalamu wabobezi wa sekta ya sheria nchini na wakufunzi kutoka vyuo vikuu hapa nchini”alisema

Aidha, alisema wakufunzi hao watatoa mada mbalimbali kwa mawakili kuhusu masuala ya sheria ikiwamo uandaaji wa mikataba, masuala ya uwekezaji, mafuta na gesi na usuluhishi wa migogoro kwa njia ya majadiliano.

Kadhalika, alisema maadhimisho hayo yatahusisha matukio mbalimbali ikiwemo mabanda ya maonesho kwa ajili ya kuelimisha umma masuala ya kisheria.

“Lengo lingine la maadhimisho haya ni Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iweze kufanya tathimini ya namna ilivyotekeleza majukumu yake ya uratibu, ushauri, usimamizi na uendeshaji mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya serikali na taasisi zake za ndani na nje ya nchi”alisema

Awali akizungumza kuhusu ofisi hiyo alisema ilianzishwa rasmi Februari 13, 2018 kupitia hati idhini ya Rais iliyotolewa kwa mujibu wa Ibara ya 36 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kutangazwa kwenye gazeti la serikali Na. 50 la mwaka 2018.

Pia, alisema maadhimisho na mafunzo hayo yanatarajiwa kuhudhuriwa na viongozi mbalimbaliwa serikali, dini na wadau wengine ikiwa ni pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mary Makondo pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi.

Alisema: “Viongozi wengine ni kutoka kutoka taasisi na idara za serikali na wadau kutoka sekta ya Mahakama hivyo natoa rai kwa mawakili wa serikali wote kushiriki kikamilifu katika matukio haya”.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto, Wazee na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima akizungumza wakati akifungua mkutano wa kitaifa wa wadau watekelezaji wa program jumuishi ya malezi na makuzi bora ya awali ya mtoto wa Tanzania, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Maofisa maendeleo jamii wahimizwa kufanya kazi zenye tija

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima amewaagiza maofisa maendeleo ya ustawi wa jamii na makatibu tawala wasaidizi kuhakikisha wanafanya kazi zenye tija ili kutekeleza mpango wa malezi na makuzi ya awali ya maendeleo ya mtoto Tanzania.

Aalitoa maelekezo hayo juzi alipokuwa akifungua mafunzo ya siku tatu ya sekretarieti za mikoa na Asasi zisiko za Kiserikali (AZAKI) zinazotekeleza Programu Jumuishi ya Taifa - Malezi Makuzi na Maendeleo ya Mtoto yaliyofanyika Jijini hapa.

Aliwataka wahakikishe watekeleza mpango huo wa kazi zao wenye tija ili malezi na makuzi yaweze kufanikishwa na mtoto alindwe katika umri wa kuanzia siku sufuri hadi miaka nane.

Pia, aliwataka wahakikishe watoto wanajengwa vyema kifikra ili kuweza kuwa na taifa lenye uwezo wa kiakili ambalo pia litakuwa na wazalishaji kiuchumi kwa taifa na kimataifa.

Katika hatua nyingine aliwataka maofisa maendeleo kuonyesha kazi zao kwa vitendo ili kuifanya jamii kuiga mambo yaliyomema na kuwatafuta mabalozi ambao watahakikisha wanapambana kuelimisha jamii jinsi ya umuhimu wa malezi na makuzi ya awali ya maendeleo ya mtoto.

Naye Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Children in Crossfire, Creig Ferla alisema kuwa iwapo watoto watapewa misingi bora na mizuri toka awali ni wazi kuwa taifa litakuwa na watoto sahihi wenye kujitambua na wenye tija kubwa katika jamii.

Alisema kuwa watoto ni tunu ya taifa na wanabeba dira ya taifa na ifahamike kuwa watoto wenye umri kati ya siku sifuri hadi miaka nane ni asilimia 67 ya Watanzania wote hivyo kati ya watu wazima nane kuna mtoto mmoja.

Hata hivyo, alisema watoto wakilelewa vema taifa litakuwa na uwezo wa uhakika wa kukuza uchumi wa nchi na taifa kwa ujumla.





# Wizara ya Afya yaweka mikakati kupunguza vifo kinamama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya imesema itaendelea kuhamasisha jamii kuhusu matumizi ya uzazi wa mpango ili kupunguza vifo vya kinamama na watoto kwa asilimia 30.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, aliyasema hayo wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023-2024 katika Baraza la Wawakilishi.

Alisema kinamama wengi hawana mwamko wa matumizi ya njia za uzazi salama wa mpangilio ambao hutoa nafasi nzuri ya ukuaji wa mtoto katika afya njema.

Mazuri alisema katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 kinamama 23,644 wapya walijiunga na njia mbalimbali za kisasa za uzazi wa mpango idadi hiyo imepunguaa ikilinganisha na kinamama 24,104 katika kipindi hicho kwa mwaka uliopita.

Alisema uzazi wa mpango hauna athari za kiafya na haupingani na dini zote kwa sababu umejikita katika kulinda afya za akinamama na mtoto aliyezaliwa kuelekea katika ukuaji mzuri

''Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watusaidie kubeba ujumbe wa uzazi wa mpango ambao umelenga kuimarisha afya za kinamama kuwa bora pamoja na mtoto aliyezaliwa kupata ukuaji mzuri,''alisema.

Aidha Mazuri alisema wizara imejipanga kutoa huduma za afya ya msingi ya akili katika jamii ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 wagonjwa ya afya ya akili 754 walisajiliwa.

Alisema katika kipindi hicho wagonjwa 438 walilazwa ambapo wagonjwa 91 wamepona na kuendelea na shughuli zao.

Hata hivyo alikiri kuongezeka kwa matatizo ya afya ya akili zaidi kwa kundi la vijana kutokana na kasi ya matumizi ya dawa za kulevya ikiwemo bangi.

Alisema: ''Mheshimiwa tunakabiliwa na tatizo kubwa la kuongezeka kwa wingi wa wagonjwa wa maradhi ya tiba ya akili ambapo kundi kubwa ni vijana na hiyo imesababishwa na sababu mbalimbali ikiwemo matumizi ya dawa za kulevya,'' alisema.

Mazrui alisema katika kuimarisha tiba ya akili Wizara ya Afya ipo katika hatua za mwisho za ujenzi wa Hospitali ya Kinyasini visiwani Pemba ambayo itatoa huduma hizo kikamilifu.

Alisema huduma za tiba ya akili kwa sasa zimeimarika kwa upande wa Unguja kupitia katika hospitali ya Kidongo Chekundu katika wodi mpya ambayo pia inatoa huduma za tiba kwa watoto.

# Ujenzi maabara ya TAEC kuongeza tija, ufanisi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUKAMILIKA kwa ujenzi wa maabara na ofisi ya Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC) visiwani Zanzibar, kutaongeza tija na ufanisi kwa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Profesa Lazaro Busagala, alisema miongoni mwa faida zitakazopatikana kwa kukamilika kwa maabara hiyo ni kuongeza tija katika utekelezaji wa sera ya taifa ya teknolojia ya nyuklia ya mwaka 2013.

Aliyasema hayo baada ya Mwenge wa Uhuru kukagua ujenzi wa maabara na ofisi hiyo TAEC huko Dunga Zuze Mkoa wa Kusini Unguja.

Profesa Busagala alisema pia kukamilika kwake kutawezesha biashara kwa wananchi wa Zanzibar sambamba na mpango wa blue print wenye lengo la kurahisisha na kuendeleza biashara nchini.

"Kuwasogezea wananchi huduma hivyo kuwapunguzia gharama za shughuli zinazohusiana na teknolojia ya nyukilia. Kwa mfano badala ya kusafiri au kusafirisha sampuli au vifaa vya kutengeneza kwenda bara kazi hizo zinaweza kufanya hapa hapa kwa gharama nafuu"alisema.

Aidha alisema pia kutasaidia sekta ya viwanda kusimamia vyema matumizi ya teknolojia ya nyuklia na hivyo kuchangia Tanzania kufikia dhamira ya uchumi wa viwanda na uchumi wa buluu.

Alisema kwa sasa kuna zaidi ya vituo 33 vya Zanzibar vinavyotumia vifaa vya mionzi katika sekta ya afya na maji hivyo kukamilika kwa maabara hiyo kutasaidia kuhakiki vifaa hivyo, kuongeza ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini pamoja na wigo wa kupata huduma hizo kutumika katika viwanda.

"Maabara hii itasaidia kuhamasisha matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia kwa kuboresha na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa usalama wa watu na mazingira"alisema.

Alisema pia kutasaidia kuimarisha ubora wa vipimo vya mionzi kwenye vyakula, mbolea, mazao ya tumbaku na sampuli za mazingira ili kudhibiti madhara ya mionzi kwa binadamu na mazingira.

Mkurugenzi huyo alisema ofisi ya Zanzibar inapima sampuli za vyakula 450 kwa mwaka na haipimi sampuli zozote za mazingira kwa sababu ya kutokuwa na uwezo huo.

"Kukamilika kwa maabara hii kutaongeza upimaji wa sampuli za vyakula hadi kufikia 790 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 175 na sampuli za mazingira zitaanza kupimwa Zanzibar," alisema.

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2023, Abdallah Shaibu Kaimu, alisema ameridhishwa na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa maabara na ofisi hiyo.

Aidha, alisema ujenzi huo umezingatia ubora, viwanngo na thamni ya matumizi ya fedha iliyotumika imeendana na ujenzi wa mradi huo.

Pia lipongeza Tume ya Atomiki kwa kazi nzuri wanazozifanya kwa pande zote mbili za muungano hivyo kuendelea kusimamia miradi yao ili kukamilika kwa wakati na miradi yenye viwango vyenye ubora.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, alisema miradi sita imekaguliwa na Mwenge wa Uhuru na mingine kuwekewa mawe ya msingi ya Sh.bilioni saba.

Ujenzi wa maabara na ofisi ya Tume ya Nguvu ya Atomiki Tanzania unatarajiwa kukamilika Julai mwakani na utagharibu Sh. bilioni tatu.




Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui akisikiliza kwa makini michango ya wajumbe wakati wakichangia bajeti ya wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makamu wa Rais atoa maagizo kwa makandarasi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla amewaagiza makandarasi na washauri elekezi kuhakikisha wanasimamia viwango na ubora wa masoko yanayojengwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Akitembelea ujenzi wa miradi hiyo jana, Hemed aliridhishwa na kasi ya ujenzi wa masoko hayo ambayo yanatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwaka huu.

Alisema kumalizika kwa masoko hayo kutatatua kero ya wananchi na wafanyabiashara ambao kwa sasa wanafanya biashara zao mazingira yasiyo rasmi hali ambayo inachangia kupotea kwa mapato ya serikali. Aidha Hemedi aliwaagiza makandarasi wa masoko hayo ambao ni Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Chuo cha Mafunzo na Kikosi cha zima Moto na Uokozi kuhakikisha ujenzi huo unakamilika kwa wakati uliopangwa na kwa ufanisi mkubwa na kuahidi kuyatembelea kila baada ya mwezi ili kufuatilia maendeleo ya ujenzi huo.

Hemed alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa kuamua kuvikabidhi vikosi vya SMZ kujenga masoko hayo jambo ambalo limeipunguzia gharama Serikali ya kuajiri makandarasi kutoka nje ya nchi.

Alisema ameridhishwa na utendaji kazi wa uongozi wa Mamlaka ya Usajili wa Majengo (ZBA) kwa kusimamia viwango na ubora wa majengo hayo.

Makamu huyo alisema serikali itaendelea na ujenzi wa miradi ya maendeleo bila ya kusita na kuwataka wananchi kuwa wavumilivu kipindi chote cha ujenzi wa miradi hiyo.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Muhamed alisema wizara yake itasimamia na kufuatilia kwa karibu ujenzi huo ili kufikia adhma ya kuwawekea mazingira mazuri wafanyabiashara yanafanikiwa.

Katibu wa Idara ya Siasa, Itikadi na Uenezi, Khamis Mbeto Khamis alisema kuwa Ibara ya 238 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwenye kifungu cha serikali za mitaa imeelekeza serikali kuhakikisha inaweka mazingira bora kwenye halmashauri kuanzia masoko na maeneo mengine kwa ajili ya wananchi.



**2PAC**
UKURASA 14



# ZUCHU IMBA, U-MISS WAACHIE WENYEWE



MWEZI Machi, waandaaji wa mashindano ya urembo, Miss Tanzania walionyesha kusikitishwa na kitendo cha msanii Zuchu kutumia taji na beji yao wakati wa utambulisho wa ngoma yake 'Napambana', bila idhini yao na kutoa taarifa, safari hii wameibuka tena, wakidai hawana tena tatizo naye, wameyazungumza na kuyamaliza, lakini wakamuonya kutothubutu tena kutumia taji, beji au nembo yao bila ruhusa yao.


Mwenyekiti wa Miss Tanzania, Azam Mwasango amesema hayo wiki hii wakati akitambulisha rasmi mashindano hayo yanayotarajiwa kufanyika hivi karibuni.

Mwasango alionya kuwa si kwa Zuchu tu peke yake, bali kwa mtu, au kampuni yoyote ni kosa kisheria kutumia taji la kichwani, beji au nembo ya Miss Tanzania bila kuwashirikisha wao na kampuni ambayo inaisimamia.

"Hauwezi kutumia taji au nembo ya mtu yeyote pasipo kumshirikisha, awali tulikuwa hatuna taarifa, tuliona tu imevaliwa, baadaye tuliwasiliana, tulizungumza nao wahusika na kila kitu kwa sasa kipo sawa. Lakini pamoja na hayo nachoweza kusema haturuhusu mtu atumie taji na nembo ya Miss Tanzania bila kupata ruhusa kwa waratibu na waandaaji wa mashindano hayo,"alisema mwenyekiti huyo.

Ilikuwa ni uzinduzi wa mashindano ya Miss Tanzania ambayo yanatarajiwa kuwashirikisha warembo 20 toka mikoa mbalimbali na kanda tofauti, wanaotarajia kupiga kambi ya wiki mbili kuanzia Juni 23.

Pamoja na kutoa onyo, mashabiki wa Zuchu na muziki wa bongo fleva wameonekana kushusha pumzi kuwa wameyazungumza na hakuna tena matatizo kwani walihofia kampuni hiyo kumpandisha msanii huyo kortini kwa kosa hilo, lakini kwa sasa wanaweza kula chakula kikashuka.



BASI SAWA

## Anjella kiki tupa kule

BAADA ya kuondoka kwenye lebo ya Konde Gang, msanii wa kike, Anjella jana alitarajia kutoa ngoma yake itakayojulikana kwa jina la 'Blessing' huku mwenyewe akisema itajiuza yenyewe, hataki kiki wala nini.

Anjella, mmoja wa wasanii wa kike wa bongo fleva mwenye sauti ya kuvutia ambaye kwa sasa yupo kivyake alitarajia kufanya ziara kwenye vyombo mbalimbali habari kuanzia jana kuitambulisha ngoma yake hiyo ambayo imekuja ghafla sana huku kukiwa hakuna kiki yoyote iliyofanywa kwa ajili ya ujio wa wimbo wake.



"Maisha yangu huwa sipendi yajulikane mitandaoni, sipendi kujionyesha, napenda kitu kikienda mtandaoni ni kwamba mimi mwenyewe nimependa kwa ridhaa yangu, na pia sipendi mambo mengi, ndiyo maana hamnioni kwenye mambo ya kiki wala nini, na siamini sana," alisema Anjella.

Mwanadada huyo aliondoka chini ya usimamizi wa Harmonize, mwishoni mwa mwaka jana na sasa ameamua kujitegemea mwenyewe.


## Country Boy hataki nguvu nyingi kutongoza

MSANII wa muziki za kizazi kipya Country Boy amesema ametumia muda mwingi kuwa bishoo na anatumia gharama kubwa kununua mavazi nadhifu ili asitumie muda mwingi kujitambulisha au kutongoza.

"Mimi kwenye maisha yangu nachukua muda mrefu kuwa smati ili nisitumie muda mwingi kuongea. Yaani nataka hata nikitokea sehemu mademu wanipende, bosi niongee naye, chunguza mabosi wengi ukiwafuata na kumwambia 'kaka samahani', anaanza kukuangalia kwanza ulivyovaa kuanzia chini mpaka juu. Sasa unatakiwa uwe na mvuto ili aweze kuongea na wewe vizuri, ndiyo maana mimi nimejitolea kuwa bishoo tu, ubishoo maana yake ni kupendeza." alisema msanii huyo.

Ameshatoa ngoma mbalimbali, kama vile 'Mateso' aliyomshirikisha Linah, 'Mia' na zingine nyingi.





# MAHARI YA ZARI HII HAPA

WAKATI kuna kinadada kibao hapa Bongo wakijishebedua kuwa wao hawaolewi kwa mahari ndogo ndogo, wengine wakitaka mamilioni ya pesa, lakini kwa mwanamama tajiri na mrembo, Zari hakutaka makuu, badala yake ameolewa kwa mahari ya kitabu tu ambacho yeye anakiamini, na ana imani ni mahari bora kuliko chochote kile ambacho mumewe Shakib Cham angetoa.

Zari ambaye ni mwanamitindo na mjasiriamali ambaye aliwasili nchini wiki iliyopita kwa inshu zake za kibiashara na kukutana na mashabiki zake Mei 27 kule Elements Masaki, Dar es Salaam, alibainisha kuwa mumewe huyo ambaye ni raia wa Uganda hakumlipia mahari yoyote ya pesa, ng'ombe au vito vya thamani kama dhahabu na fedha, badala yake yeye alitaka kitabu tu cha imani ambayo anayoiamini kwani anaona ndiyo kitu kikubwa zaidi kuliko vyote.

"Ndoa umefungwa, lakini kwa sasa najiandaa kufanya pati kubwa ya kifahari ambayo watu wote wataiona," alisema mwanamama huyo ambaye ni mzazi mwenzake staa wa muziki wa Kibongo kwa sasa, Diamond Platnumz.

Ndoa ya hao wawili ilifungwa kiasi cha mwezi mmoja na kitu uliopita, huku baadhi ya mashabiki, mitandao na magazeti wakielezea utofauti wa miaka 12 kati yake ya mkewe.

Wakati Zari kwa sasa akifikisha umri wa miaka 42, mumewe ameripotiwa kuwa na miaka 30, hivyo Zari kumpita mumewe umri wa miaka 12, lakini haiondoi ukweli na uhalali wa ndoa, hivyo ni mke na mume na wenye wivu wajinyonge.





# Marlaw afunguka kifo cha 'Rita'

MOJA ya wasanii wa mwanzo wa muziki wa bongo fleva, Marlaw, hatimaye ameibuka mafichoni na kusema kuwa wimbo wake matata uliotikisa anga la muziki wa kizazi kipya 'Rita' lilikuwa ni tukio la kweli lililomtokea mmoja wa mashabiki wake.

Marlaw ambaye alitoa wimbo huo katikati ya miaka ya 2000 na kumfanya kuwa maarufu zaidi, alisema ilitokea kama bahati tu kutunga wimbo huo kwani kisa hicho alisimuliwa na shabiki wake mara baada ya kuukubali wimbo wake wa 'Bembeleza'.

"Kuna mtu alifurahia sana wimbo wa 'Bembeleza,' akaona naweza kuandika hata wimbo unaomhusu yeye, akanifuata shabiki huyo akaniambia nina historia yangu kuna kitu kilinipata mimi mwenyewe, naamini ukitengenezea wimbo utakuwa mzuri sana, basi akanisimulia, kusema kweli mimi nikavutiwa sana na stori yake, ndiyo nikatengeneza 'Rita.'"

Anadai kuwa sasa amekuwa akifuatwa na watu watengeneza filamu na maprodyuza ili awape ruhusa ya kutengeneza filamu inayohusu tukio hilo, huku mwenyewe akiweka wazi kuwa hawezi kumkataza yeyote kufanya hivyo.

Nimewahi kukutana na watu wa filamu, kuwa hii stori yako hatuwezi kuitengenezea filamu, wafanye tu, mimi sidhani kwangu ni shida, wanaweza kufanya bila ruhusa kwa sababu mimi nimeshatoa wimbo, jambo langu tena hili la wananchi wote na jamii nzima," alisema mkali huyo.

# WAPIGAJI WA5 ALA PENDWA YA MAGUFULI

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE muziki hasa wa dansi kuna chombo kinaitwa tumba au conga. Hizi ni ngoma mbili au tatu ambazo huchanganywa na vyombo vingine kama magitaa, drums, kinanda, trumpet, saxaphone na vingine ambavyo vikipangiliwa kwa pamoja kwa ufundi wa hali ya juu, hutoa wimbo au muziki ambao huburudisha kwenye mioyo ya binadamu.

Kwa wale wasiojua tumba ni zile ambazo Rais wa Awamu ya Tano, hayati Dk. John Magufuli alizokuwa akizikung'uta wakati wa uhai wake akienda kwenye hafla yoyote na kukuta bendi ya muziki wa dansi. Alikuwa akimaliza shughuli zake anakwenda kuzipiga kwa ustadi wa hali ya juu.

Kiasili tumba ni ngoma za kawaida tu kama zile za kiasili, ila zile zinazoonekana kwenye bendi ziko za aina mbili. Kuna zingine ni ngozi ya wanyama, lakini zingine zimetengenezwa kiwandani kwa kutumia vitu kama ngozi au plastiki laini, lakini mlio wake ni kama ngoma za kawaida.

Kazi yake ni kuweka vionjo ili muziki uvutie zaidi hasa kwa muziki wenye mahadhi ya kiafrika.

Tanzania imepata kuwa na bahati ya wapiga tumba waliokuwa na uwezo mkubwa wa kuzikung'uta na kufanya burudani kwa mashabiki si kwa midundo tu, bali hata mbwembwe zao wawapo jukwaani.

Leo tunawaangalia wapiga tumba au conga waliotamba wakiwa na bendi mbalimbali nchini.

**1. CD Morris**

Ni mmoja wa wapiga tumba mahiri ambao Tanzania ilibahatika kuwa nao. Alitamba sana kuanzia katikati ya miaka ya '70 hadi mwanzoni mwa miaka ya '90 alipofariki dunia.

CD Morris, alianzia na Safari Trippers na kuzunguka bendi mbalimbali, ikiwemo Juwata Jazz Band 'Msondo Ngoma', 'Maquiz Du Zaire' na hadi anafariki dunia alikuwa kwenye bendi ya MK Group.

Ukizisikiliza nyimbo ambazo amepiga tumba, utagundua kuwa alikuwa na kipaji cha aina yake, kwani anavyozipiga unaweza ukadhani ni iliyopiga ni mashine na si mikono ya mwanadamu.

Pia alikuwa na mbwembwe jukwaani kiasi cha mashabiki kumzunguka na kumkodolea macho kwa mshangao badala ya kucheza muziki.

**2. Ally Jamwaka**

Inabidi Tanzania ijivunie kuwa na mwanamuziki kama huyu, kwani ni mmoja wa wapiga tumba wachache mahiri ambao bado wako hai.

Ally Jamwaka, ana uwezo mkubwa wa kutumia tumba na wakati mwingine akipiga utazisikia zikisikika wazi kana kwamba ngoma ya mdundiko hivi.

Kwa kipindi kirefu cha maisha yake ya muziki amepigia DDC Mlimani Park Orchestra na Vijana Jazz.

**3. Mohamed Chomachoma**

Hana bahati tu kujulikana au kupata sifa kwa mashabiki wa muziki, lakini wanaohudhuria bendi mbalimbali wanamfahamu mwanamuziki huyu kuwa ni mmoja wa wakung'uta tumba kwenye kiwango cha hali ya juu, pamoja na machachari yake jukwaani hufanya muziki uchangamke kupita kiasi.

Mohamed Chomachoma alipachikwa jina la 'mikono ya tembo' na hayati Tx Moshi William alipokuwa na bendi ya Msondo Ngoma. Mbali na Msondo, kipaji chake kilianza kuonekana kwenye bendi ya Diamond Sound Wana Dar es Salaam Kibindankoi, Dar Mosica na FM Academia.

**4. Mohamed Haroub**

Alikuwa mpiga tumba mahiri wa bendi ya Uda Jazz kiasi cha bendi kubwa kama Juwata Jazz kumchukua kwenye miaka ya '80.

Haroub ambaye ni marehemu kwa kiasi kikubwa ndoye aliyepiga nyimbo nyingi kuanzia miaka ya '80 hadi mwishini mwa miaka hiyo.

**5. MCD**

Kwa kizazi cha miaka ya hivi karibuni watamkumbuka mpiga tumba huyu mahiri, aliyekuwa akipiga kwa mbwembwe huku mdomoni akiwa na filimbi.

FILAMU

# Batuli: Ukisema cha nini...

**Na Adam Fungamwango**

UKISEMA cha nini wenzio wanajiuliza watakipata lini. Ni moja ya misemo inayofundisha kuwa unaweza ukawa na kitu ambacho kwako unaona cha kawaida tu, hukitilii maanani, unakichukulia poa na kukidharau kwa sababu kiko mikononi mwako, lakini kuna wengine ambao hawana wanakihitaji kwa udi na uvumba. Wanaomba Mungu siku isiyo na jina wakipate.

Dunia ndivyo ilivyo na jamii yetu imekuwa ikikumbana na kitu kama hiki kinachoitwa mazoea. Usifanye mazoea kwenye kitu cha thamani.

Twende kuanzia mwanzo hadi mwisho kwenye filamu hii itwayo 'Batuli.' Inakufundisha kitu na unaweza kushtuka, ukabadilika.

Imechezwa na wasanii Christina James, Adam Leo, Mariam Ibrahim, Waison Kulindwa na wengineo.

Batuli ni msichana mrembo ambaye anaishi na mumewe Wilson. Mwanaume huyo amemtoa mbali kijijini na kumleta mjini ambapo hana ndugu yeyote. Ingawa alitoa baadhi ya mahari, lakini bado hawajafunga ndoa.

Maisha hayakuwa mazuri kwa Batuli kwani mumewe akawa na tabia ya kumpiga, kumnyanyasa na kumdharau. Upande wa pili wa shilingi kuna kijana aitwaye Adam, halali wala hashibi kwa ajili ya Batuli.

Mara kwa mara hukutana naye akienda kisimani. Humsalimia na kumsimamisha, lakini Batuli anakuwa mkali kwa ajili ya kulinda nyumba yake.

Pamoja na hayo, ndani ya nyumba kukawa kunawaka moto, hakuna furaha wala nini. Mume mlevi, anarudi nyumbani anavyotaka yeye. Akawa sasa anamfanya kama mtumwa badala ya mke.

Siku ya siku akamletea mwanamke nyumbani na kumtimua. Hakujua pa kwenda. Alikokwenda alikutana na vibaka wakampora mfuko wa nguo pamoja na simu yake ya mkononi. Akajikuta amekaa sehemu kwenye nyumba mbovu. Adam akapita na kumkuta kwenye hali ile. Alipomuuliza akamhadithia yote, hakutaka kumficha kitu. Adam akamchukua na kwenda kumhifadhi kwake. Kesho yake akamfuata Wilson na kumwambia amsamehe mkewe ili warudiane. Hakupata ushirikiano kwani alionekana hamtaki tena mwanamke mwenyewe.

Akarudi na kujikalia na Batuli. Wilson alikuwa amechukua mwanamke ambaye kunguru asiyefugika. Siku si nyingi akamtoroka na kuchukua kila kitu cha ndani.

Akamkumbuka mkewe, akaamua kwenda kwa Adam, ikiwa ni baada ya miezi sita tangu kumtimua. Alipofika akamkuta Adam na kumwambia amekuja kumchukua mkewe. Adam akamwita Batuli. Wilson alipomuona akashtuka na presha ikampanda. Tayari Batuli alikuwa mjamzito.






# Tupac ahera, tuzo duniani

LICHA ya kufariki takriban miaka 27 iliyopita, aliyekuwa rapa maarufu duniani Tupac Shakur ametunukiwa tuzo kama nyota kwenye Hollywood Walk of Fam.

Kwa mujibu wa chombo cha habari cha CBS, alisema tuzo hiyo itatolewa kwenye sherehe inayotarajiwa kuandaliwa baadaye mwaka huu na kampuni iliyotoa tuzo hiyo.

Imeelezwa kuwa mwigizaji maarufu wa redio Big Boy, atashiriki hafla hiyo wakati wazungumzaji waalikwa watajumuishwa kwenye hafla hiyo, akiwemo Mkurugenzi wa kampuni iliyotoa tuzo, Allen Hughes na dadaake Tupac, Sekyiwa Shakur, ambaye atapokea tuzo nyota huyo kwa niaba ya kaka yake.

Rapa huyo aliuawa Septemba 23, 1996 akiwa na miaka 25 tu, siku kadhaa baada ya kushuhudia pambano la ngumi kati ya Mike Tyson dhidi ya Bruce Seldon huko Las Vegas, Nevada, nchini Marekani lililofanyika Septemba 7 mwaka huo.



## Kodak utaua watu kwa raha

RAPA wa Kimarekani Kodak Black ametoa albamu yake mpya iitwayo'Pistolz & Pearlz', ikiwa na ngoma 21.

Msanii huyo ambaye jina lake halisi ni, Bill Kahan Kapri imekuwa ni albamu yake ya tano ambayo ilikuwa inasubiriwa kwa hamu kubwa na mashabiki wake na muziki huo kwa ujumla, huku mwenyewe akithibitisha kwenye mitandao ya kijamii.

"Asante kwa kila mtu ambaye amekuwa katika safari hii, nisingeweza kupata amani na hakuna kitu kikubwa ila ni heshima na shukrani," aliandika msanii huyo.

Ingawa mara nyingi ngoma amekuwa akizifanya peke yake, lakini kwenye albamu hii amewashirikisha mastaa wengine kibao kama vile EST Gee, Loe Shimmy, Lil Crix na VVSNCE.

## Kansa inamtafuna Adolfu

Watoto au vijana wa miaka ya 1980, na 1990, wanamkumbuka staa mmoja mwigizaji wa filamu za ubabe, mapigano na silaha, wenyewe wakimwita 'Adolfu.'

Mbabe huyu ambaye jina lake halisi ni Dolph Lundgren, kwa sasa anapambana na ugonjwa wa saratani akiwa na miaka 65.

Alisema kuwa ugonjwa wake huo uligunduliwa mwaka 2015, na alipata nafuu lakini mwaka 2020 ugonjwa ukamchachamalia tena kiasi cha kuambiwa daktari mmoja kuwa alikuwa amebakisha miaka miwili au mitatu ya kuishi.

'Ni siku moja baada ya upasuaji wangu, waligundua kuwa kulikuwa na mwingine zaidi kuzunguka eneo hilo la uvimbe wa kwanza, nikawauliza nimebakiza muda gani, nadhani daktari alisema miaka miwili au mitatu," alisema staa huyo raia wa Sweden.





## Beyonce amlilia Tina Turner

Msanii mwimbaji wa Kimarekani, Beyonce alitumia nafasi kwenye ziara yake ya Renaissance nchini Uingereza kumkumbuka mwanamuziki mkongwe Tina Turner aliyefariki dunia Mei 24 akiwa na miaka 83, akisema ndiye aliyekuwa 'role model' wake kwenye muziki.

Akiwa kwenye onyesho lake wiki hii lilioitwa, 'queen of all time Beyonce,' alitoa salamu zake za rambirambi kwa ndugu, familia, jamaa na marafiki wa marehemu kutokana na msiba huo mzito, akiwa kwenye Uwanja wa Tottenham Hotpur, Kaskazini mwa London.

Alisema kama wasanii wengi, alipatwa na mshtuko na simanzi kubwa, alipopokea habari za kifo cha Turner.

"Malkia wangu kipenzi, nakupenda bila kikomo, nashukuru sana kwa msukumo wako, na njia zote ulizofungua, wewe ni nguvu na za kuigwa, sote tumebahatika kushuhudia wema wako na roho nzuri ambayo itatusaidia kubaki milele. Asante kwa yote uliyofanya, alisema aliomboliza Beyonce."

## LIL Durk kamua twende

LIL Durk, yule rapa wa Kimarekani, jina lake kamili likiwa ni Durk Derrick Banks, ameachia albamu mpya kabisa wiki hii iitwayo 'Almost Healed' akiwashirikisha mastaa kibao.

Hii inakuwa ni albamu yake ya 13, tangu alipotoa ya kwanza iliyoitwa 'Remember Bay Name', mwaka 2010.

Rapa huyo mwenye miaka 30, ametoa albamu hiyo yenye zaidi ya nyimbo 20, akiwa amewashirisha nyota wengi wakali kwenye ngoma tofauti ili kuweka ladha mchanganyiko kama J Cole, Future, 21 Savage, Kodak Black, Morgan Wallen, Alicia Keys, Southside, Metro Boomin, Zaytoven, Wheezy, Cubeatz, na ngoma nyingie iitwayo 'Cross the Globe' ambaye alimshirikisha msanii ambaye kwa sasa ameshafariki dunia Juice WRLD.






Meneja Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) Kanda ya Kaskazini, Vones Koka (kulia), akiwahudumia wanachama wa Mfuko huo waliotembelea banda la PSSSF katika Maonyesho ya Biashara na Utalii kwenye viwanja vya Mwahako, jijini Tanga mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# TANSHEP waleta neema kwa wakulima wa mboga

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WAKULIMA wanaojishughulisha na kilimo cha mboga katika Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru wameanza kunufaika na programu ya 'anzia sokoni malizia shambani kwa kipato zaidi' kupitia mradi wa TANSHEP, unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA).

Mradi huo umelenga kuwasaidia wakulima wadogo kwa kuanza na utafiti wa soko na kujua nani atamuuzia bidhaa yake.

Baadhi ya wakulima katika Kata za Bangata na Sambasha, wakizungumza na Nipashe wakiwa kwenye mashamba yao, walisema wameanza kunufaika na programu hiyo.

Neema Mathayo ni mkulima wa mboga Kijiji cha Midawe Kata ya Bangata, alisema walipata mafunzo ya kufanya utafiti wa kuanzia sokoni kwa kutafiti bei za mazao kwa msimu husika kabla ya kuamua kulima na kubadilisha kilimo kwa kukifanya kuwa cha biashara na kiendane na uhalisia wake.

"Tumelima viazi kwa kufanya utafiti wa soko kabla ya kulima, kipindi tutakapovuna uhitaji wa viazi utakuwa mkubwa kwa kuwa bei yake itakuwa kubwa, pia tumelenga msimu mzuri kwa soko,"alisema Neema.

Naye Joel Labarani, alisema kuwa program hiyo imewasaidia wakulima kulima kilimo cha kisasa kinachoendana na mahitaji ya soko na kuwaondoa kwenye kilimo cha mazoea cha kulima tu ilimradi wameotesha mazao shambani.

Dina Erasto, mkulima katika Kata ya Sambasha, alisema kupitia progamu hiyo angalau imeanza kupunguza madalali wa mazao ambao waliwanyonya kwa muda mefu.

Alisema kwa sasa wakulima wana mawasiliano ya moja kwa moja na wafanyabiashara sokoni hivyo anafanya uamuzi wa kumuuzia dalali mazao yake au kwenda mwenyewe sokoni kwa kuangalia bei halisi iliyoko kwa wakati huo.

Mkulima mwingine, Ester Michael, alitumia fursa hiyo, kuishukuru serikali kupitia watalamu wa kilimo ngazi ya kata na Halmashauri ya Arusha, kwa kuwa na wakulima bega kwa bega, kuwapa ushauri wa kitaalamu pamoja na kuwaunganisha na wadau wengine wa kilimo, masoko na ujasiriamali ambao unawawezesha wakulima kuendelea kufanya kilimo biashara.

Mkuu wa Kitengo cha Kilimo wa Halmashauri hiyo, Bahati Mtweve, alisema utekelezaji wa program hiyo ni mkakati wa serikali kwa kuwa ya agenda ya kilimo biashara.

Alisema: "Kwa sasa wakulima wameanza kunufaika na kilimo kwa kulima zao kulingana na mahitaji ya soko na pia kuuza mazao yao kwa kuzingatia bei ya soko bila kunyonywa na wachuuzi".

Halmashauri ya Arusha kupitia idara ya kilimo kwa kushirikiana na wadau wa kilimo wanaendelea kutoa mafunzo ya utaalamu wa kilimo kwa wakulima husasani kilimo cha kisasa kitakachowaletea kipato zaidi na kufikia ajenda ya kilimo biashara.

# NEMC yaziagiza halmashauri kupanda miti

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MENEJA wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC), Kanda ya Kaskazini, Lewis Nzali, ameziagiza halmashauri zote katika ukanda huo kuhakikisha wanapanda miti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kulinda vyanzo vya maji.

Alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na Nipashe ikiwa ni kuelekea maadhimisho ya wiki ya mazingira.

Kiongozi huyo alisema endapo halmashauri hizo zitazingatia agizo hilo itasaidia kurejesha uoto wa asili pia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Hata hivyo alisema kila halmashauri imepewa jukumu la kuotesha miti milioni 1.5 kila mwaka kwa kurudisha uoto wa asili uliopotea pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Licha ya kuzungumza hayo alizitaja halmashauri zinayofanya vizuri katika shughuli ya upandaji wa miti kuwa ni Halmashauri ya Meru kuwa imekuwa ikijitahidi kuhamasisha kwa vitendo kila mwaka.

Aidha alizitaka halmashauri nyingine na taasisi mbalimbali kuendelea na zoezi la kuotesha miti ili kufikia malengo yaliyowekwa na serikali.

"Kila halmashauri ikiweza kufikisha lengo la kuotesha miti iliyokusudiwa ambayo ni milioni 1.5 kwa kila mwaka hakika tutapiga hatua na kufika mbali na tutafanikiwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. "Kwa kuwa vyanzo vingi vya maji vinatoka Meru naona ni moja ya sababu inayochangia zaidi wao kuendelea kutekeleza suala hilo la kupanda miti kwa wingi ila napenda kutoa wito kwa halmashauri nyingine kuiga mfano huu," alisema Nzali.

Alisema NEMC imekuwa ikitoa elimu kwa taasisi zikiwamo shule na watu binafsi kupanda miti ili kutunza mazingira na mwaka 2022 walikuwa na kampeni kwa kila mwanafunzi kupanda mti mmoja na kutunza.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Meru, Zainabu Makwinya, alisema wamekuwa wakihamasisha upandaji miti kwa vitendo kwenye halmashauri hiyo kwa kuwa kwa mwaka jana wamefanikiwa kupanda miti zaidi ya milioni 1.3 na wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na wadau wa mazingira.

"Hatufanyi peke yetu bali tumekuwa tukishirikiana na wadau wa mazingira kuhakikisha kuwa kila Kata ya Meru miti inapandwa na bado tunaendelea kuhamasisha zaidi kupanda miti zaidi," alisema Makwinya.

# Wataalamu wakutana kujadili uboreshaji miundombinu

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof.Makame Mbarawa, amesema wataalamu wa barabara kutoka nchi mbalimbali wamekutana jijini Arusha kwa ajili ya kujadiliana namna ya kupunguza uchafuzi wa mazingira na uboreshaji miundombinu ya barabara.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati akifungua mkutano huo, Waziri Mbarawa, alisema barabara ni kitu chenye umuhimu hasa kwenye usafirishaji mizigo, hivyo wataalamu wamekutana kwa lengo la kuzungumzia matatizo kwa ajili ya kupunguza msongamano na uchafuzi wa mazingira.

"Tumekutana na wataalamu mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi, wako wanaotoka Bara la Asia, Ulaya na baadhi ya nchi za Afrika, tumekuja kubadilishana ujuzi wa namna ya kupunguza msongamano barabarani kwa kuwa faida zinazotokana na barabara ni kubwa kwa kuwa asilimia 90 ya mizigo inasafirishwa kupitia barabara,"alisema Mbarawa.

Hata hivyo, alisema kama serikali inaangalia namna ya kuhamishia usafirishaji wa mizigo kutoka barabarani kwenda kwenye reli kwa kuwa serikali inajenga Reli ya Kisasa (SGR), ila kwa sasa barabara bado ndiYo mhimili mkuu wa usafirishaji.

Mmoja wa washiriki wa mkutano huo, Lidya Chira, ambaye ni Meneja wa Masoko wa Kampuni ya CAMEA, inayosimamia masuala ya barabara nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), alisema barabara zikijengwa kwa kiwango kizuri ni dhahiri itadumu kwa muda mrefu na itapitisha magari ya kila aina bila kujali ukubwa.

"Ni vyema wataalamu wa ujenzi wa barabara wakafanya ujenzi wa kisasa na bora na unaoaminika na wasifanye kwa ajili ya muda mfupi bali watumie malighafi sahihi ili ziwe imara na zenye kudumu muda mrefu,"alisema Chira.

Mkutano huo pia ulilenga kujadili masuala ya usafirishaji wa mizigo kwa barabara na namna sekta hiyo itachangia maendeleo ya uchumi wa jamii na taifa kwa ujumla.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Enzi hizo mdundiko ukipita mtaani watoto hupotea, kinamama kuunguza mboga

**Na Adam Fungamwango**



LEO tupo kwenye maeneo ya Pwani, kama vile Dar es Salaam, Bagamoyo, Kisarawe, Kibaha na mengine yanayofanana na hayo, ambapo kulikuwa na ngoma maarufu ya mdundiko.

Ilikuwa ngoma maarufu sana miaka ya 1980 hadi 1990. Ingawa hadi leo ipo, lakini imepungua nguvu na umaarufu hasa sehemu za mijini hususan Dar es Salaam.

Ngoma hii ilikuwa maarufu sana kwenye sherehe za kiserikali na kijamii, kama vile harusi, jando, kipaimara, komonio, na hata wakati wa hafla za viongozi wanapotaka kuhutubia.

Ni ngoma ya asili ya Wazaramo wa mkoa wa Pwani, ambayo miaka niliyoitaja ilikuwa ikipita sehemu, inazoa idadi kubwa ya watu na kuondoka nayo hadi itakapokwenda kufikia.

Wapigaji walikuwa na ngoma kubwa ambayo ndiyo kinogesho cha ngoma yenyewe. Inafungwa kamba ambayo mpigaji anaivaa mabegani kwa sababu ni kubwa na nzito.

Kuna mpiga debe, halafu mpiga manyanga, ngoma moja ndogo inayopigwa pande zote mbili kwa kutumia mkono maarufu kama 'kidalidali', pamoja na vitatarizi vingine ambavyo wenyewe wataona vinafaa.

Wengi waliokuwa wanasombwa na ngoma hiyo, ni wanawake na watoto. Staili ya ngoma hii haikai sehemu moja.

Ni ngoma inayotembea. Inaweza kutoka Ilala ikaenda hadi Msasani. Mbagala hadi Buguruni. Magomeni hadi Kunduchi au Boko. Inakatiza barabara na mitaa yake.

Kila inapopita, akinamama wanatoka majumbani kwao ili kuangalia, kucheza, au kuondoka nayo moja kwa moja wakicheza na kuburudika. Watoto nao ni hivyo hivyo.

Itoshe kusema tu kuwa ilikuwa inachukua umati mkubwa na watu kiasi kwamba unaweza kupotezana na mtu hapo hapo kwenye ngoma na usimuone tena, hapa umtafute vipi.

Kwa kiasi kikubwa ilikuwa inaleta burudani kwa jinsi wanavyopita, wanavyokatiza mitaa, huku kukiwa na kundi kubwa la watu mara kumi au zaidi la hawa wa sasa wa kigoma cha 'uruguay', 'mduara' au 'kigodoro.',

Aina ya uchezaji wa akinadada wa wakati huo, ambao walikuwa wakisakata huku wakizurura nayo ilivutia na kuburudisha zaidi.

Awali sikuwa najua ni kwa nini mdundiko huwa unatembea na haukai sehemu moja kama ngoma zingine.

Lakini baadaye nilipokuja kuwa mkubwa kidogo, niligundua kuwa kumbe ngoma hiyo ilikuwa inakodishwa, na kule kutembea ni kwamba wapiga mdundiko walikuwa wakitoka kwenye makao makuu yao na kuelekea kule walikokodishwa, iwe kwenye sherehe, mkutano au hafla.



Na hata wakati wa kurudi kwao pia walikuwa wakipiga na kutembea, kutoka walikoalikwa baada ya kumaliza sherehe.

Kwa wakati ule vikundi havikuwa vingi sana vya ngoma hiyo, baadhi yao kulikuwa ni kama 'Kikundi cha Taifa', chenye maskani ya Buguruni 'Joka Kuu', kilikuwa Mwananyamala na vingineo.

Akinamama mfano wa Kinondoni wakienda Buguruni kukodisha, wao hawaweki ngoma zao mabegani hadi wafike eneo husika, au kukodishiwa magari kama hawa wa sasa, la hasha. Wanaanza kupiga kuanzia hapo hapo kwenye makao makuu yao na kuanza kuondoka na akinamama wahusika waliowakodisha, iwe wawili au watatu hadi wanakokwenda walikokodishwa.

Sasa huko njiani ndiyo balaa. Kila wanapokatiza wanapata watu wa kuondoka nao.

Vijana wa mjini wa sasa wanasema 'wanasepa na kijiji'. Hadi wafike kwenye sherehe mdundiko unakuwa umepeleka idadi kubwa ya watu ambao hawajaalikwa. Kizuri ni kwamba zamani hakukuwa na kadi wala barua ya mwaliko.

Yeyote yule anayekuwepo ndiyo mwalikwa. Na kwa uchunguzi wangu mdogo niligundua kuwa wanapofika kwenye sherehe, hafla, au mkutano haipigwi tena staili ile ya mdundiko.

Wanapokuwa wamekaa chini wanapiga staili au ngoma ya vanga na si mdundiko tena. Nadhani ilionekana utamu wa ngoma ya mdundiko ni kule kutembea kwenyewe na kukatiza mitaa na barabara.

Pamoja na burudani ya aina yake, kuna athari zilikuwa zikipatikana kutokana na ngoma hiyo.

Nayo ni kupotea kwa watoto. Pia ni wanawake kuunguza mboga na wakati mwingine kuingia mzozo na waume wao, ikiwemo kupigwa.

Watoto waliipenda sana ngoma hiyo. Na kila ikipita ni lazima aunganishe na kuzurura nayo.

Tatizo wanapochoka na kujitoa kwenye kundi, wakajikuta wapo mbali na nyumbani, na hawajui njia waliopitia hadi kufika hapo.

Kifupi tu ni kwamba wanakuwa wamepotea.

Hata wale wanaofika mwisho kwenye sherehe, pia wanakuwa hawawezi kurudi walikotoka. Wazazi wanapata shida ya kuwatafuta.

Hadi kupatikana ni lazima kazi kubwa ifanyike, au vituo vya polisi vihusike. Wakati huo simu hakuna.

Kwa upande wa akinamama hao hawapotei. Tatizo ni kwamba wakati mwingine wanakuwa wamebandika mboga, nyama au maharage. Mdundiko unapita.

Anakimbilia, anacheza au kufuatana nao kwa robo, nusu au kilometa moja.

Akirudi nyumbani mboga imeungua. Pata picha mumewe akirudi inakuwaje. Wakati mwingine hata kama hajaacha mboga jikoni, akirudi anamkuta mumewe amesharejea kazini.

Nyumbani hakukuta mtu. Mke hata akijitetea alifuata ngoma, bado haamini-ki. Wakati mwingine mama amefuata ngoma mlango ameacha wazi, vibaka wanafanya yao.

**Kwa maoni 0716 350534**

# Rais Biden aanguka jukwaani

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Joe Biden, amejikwaa na kuanguka jukwaani wakati wa uzinduzi wa sherehe za Chuo cha Jeshi la wana Anga la nchini humo huko Colorado, huku Ikulu ya Marekani ikieleza kuwa kiongozi huyo yuko sawa.

Kwa mujibu wa CNN iliyonukuu taarifa ya Ikulu ya Marekani iliyotolewa jana, Rais Biden baada ya kumaliza hotuba yake ya uzinduzi katika mahafali ya chuo hicho cha wana anga alijikwaa alipokuwa akijaribu kukimbia kutoka jukwaani.

"Haraka sana, askari kadhaa na wahudumu wake wa usalama walimkimbilia rais huyo ili kumsaidia kuamka na kurudi mahali pake, huku waliokuwepo katika sherehe hiyo wakipiga makofi," ilisema.

Iliongezwa kuwa baada ya tukio hilo, rais huyo wa Marekani alielekeza kidole kwenye sakafu ya jukwaa ambalo alisema ni chanzo cha yeye kuanguka baada ya kujikwaa.

Pia ilisema Rais Biden alirudi kwenye kiti chake bila msaada, na alionekana mwenye furaha wakati sherehe inahitimishwa.

"Yuko sawa, kulikuwa na mfuko wa mchanga jukwaani alipokuwa akipeana mikono," Mkurugenzi wa Mawasiliano Ben LaBolt aliandika kwenye mtandao wa Twitter.

Aidha, ilielezwa kuwa tukio hilo la kusikitisha la Rais Biden (80), ambalo linaonekana kuwa si la kawaida, tayari linachochea mjadala kuhusu umri wa rais huyo, mgombea katika uchaguzi wa urais mwaka 2024, ambao wafuasi wa Donald Trump (76), wamekuwa wakikosoa.

**RFI**



Wasaidizi wa Rais wa Marekani, Joe Biden wakimsaidia kumuinua baada ya kujikwaa na kudondoka jukwaani, juzi. **PICHA: MTANDAO.**

# BRICS yajadili uwezekano wa kujitanua

**MOSCOW,** RUSSIA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Lavrov amekutana na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Ma Zhaoxu pamoja na wanadiplomasia wengine wa ngazi ya juu wa Jumuia ya Nchi Zinazoendelea Kiuchumi (BRICS) ili kujadili uwezekano wa kujitanua kibiashara. Ilielezwa kuwa mkutano huo wa wanadiplomasia wa BRICS uliangazia uwezekano wa jumuia hiyo kujitanua na kuzijumuisha nchi zinazosafirisha mafuta kwa wingi duniani, ikiwemo Saudi Arabia, Iran na Umoja wa Falme za Kiarabu.

Kabla ya mazungumzo hayo yaliyofanyika juzi katika Cape Town, Afrika Kusini, Lavrov aliiweka BRICS ambayo kwa sasa inazijumuisha nchi za Brazil, Urusi, India, China na Afrika Kusini, kama msingi wa kuanzishwa kwa utaratibu wa haki zaidi ulimwenguni.

Ilielezwa kuwa Lavrov pia aliyakosoa mataifa ya Magharibi kutokana na vikwazo vyake pamoja na kile alichokiita hujuma za vitisho katika soko la fedha dhidi ya Russia.

"BRICS ina muundo tofauti, ni shirika jipya linalozingatia kanuni za usawa, kuheshimiana, maafikiano na kutoingiliana, jumuia hii inazingatia kikamilifu mkataba wa Umoja wa Mataifa (UN), kwa kufuata kanuni zake zote za kuanzisha jumuia," alisisitiza Lavrov.

Wakati huo huo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Afrika Kusini, Naledi Pandor mwenyeji wa mkutano huo, alithibitisha kuwa Rais wa Russia, Vladmir Putin alialikwa Afrika Kusini katika mkutano wa kilele wa BRICS utakaofanyika mwezi Agosti mwaka huu, licha ya Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu, ICC kutoa waranti ya kukamatwa kwake.

Mkutano huo wa mawaziri wa mambo ya nje wa Russia, Brazil, India, Afrika Kusini na China, ulikuwa maalum kwa ajili ya kuandaa mkutano wa kilele wa wakuu wa nchi za BRICS utakaofanyika mjini Johannesburg, na umefanyika chini ya wiki mbili baada ya mkutano wa kilele wa viongozi wa kundi la mataifa saba yaliyoendelea zaidi kiuchumi duniani, G7 nchini Japan.

Pia ilibainishwa kwamba kuongeza vikwazo dhidi ya Russia kama adhabu kutokana na uvamizi wake nchini Ukraine na kutafuta njia za kukabiliana na ushawishi wa kiuchumi wa kimataifa wa China ulimwenguni kulitawala mkutano huo wa G7 uliofanyika Hiroshima.

Lavrov alisema kutokana na hali iliyojitokeza ya hatua zilizochukuliwa na nchi za Magharibi, nchi zao zinapaswa kutafuta kikamilifu majibu ya pamoja kwa changamoto za wakati huu.

Alisema kutokana na ushiriki wa Russia na China, BRICS inazidi kutazamwa kama kigezo kinachoibuka kwa G7 na mataifa ya Magharibi, na upanuzi wa jumuia hiyo unaweza kuimarisha ushawishi wa kisiasa na kiuchumi wa mataifa hayo mawili.

Balozi wa Afrika Kusini katika jumuia ya BRICS, Anil Sooklal alisema zaidi ya nchi 20 zimeomba rasmi na kwa njia isiyo rasmi kujiunga na jumuia hiyo, na kwamba Saudi Arabia, Iran na Umoja wa Falme za Kiarabu kila mmoja ametuma maombi rasmi ya kujiunga na BRICS.

Ilielezwa kuwa mawaziri wa mambo ya nje kutoka kwenye takribani nchi 15, baadhi yao zikiwa zilizoomba kuwa wanachana wapya wa BRICS, walialikwa katika siku ya pili ya mkutano wa wanadiplomasia wa jumuia hiyo.

**DW**

# Marekani yatangaza vikwazo kwa wanaozozana Sudan

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imetangaza vikwazo dhidi ya viongozi wa Sudan wanaopigania madaraka, ikiwalaumu kwa kukwamisha makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyopatikana chini ya juhudi za Marekani na Saudi Arabia.

Ilielezwa kuwa Marekani ilitangaza vikwazo hivyo juzi, baada ya mashambulizi ya makombora ya anga kuua raia 18 katika soko moja mjini Khartoum ambako mapigano yaliendelea baada ya Jeshi la Sudan kujiondoa kwenye mazungumzo ya amani.

Kwa zaidi ya wiki sita, Khartoum na maeneo mengine ya nchi hiyo yamekumbwa na vita vya umwagaji damu kati ya jeshi na kikosi cha Rapid Support Forces (RSF), huku Washington ikisema pande hizo mbili zimehusika kwa kuvunja makubaliano ya kusitisha mapigano na kuchochea umwagaji damu wa kutisha.

Katika taarifa iliyotolewa na mshauri wa masuala ya usalama wa taifa Jake Sullivan, alisema "Tunafuatilia hali hiyo kwa kuweka vikwazo na vizuizi vya visa dhidi ya wahusika ambao wanaendeleza ghasia."

Kamati ya wanasheria wa haki za binadamu ilisema "Raia 18 waliuawa na 106 kujeruhiwa kwa shambulio la makombora na mashambulizi ya mabomu na ya anga Jumatano katika soko kusini mwa Khartoum."

Hata hivyo, inaelezwa kuwa asilimia kuwa ya watu wanaojiweza kiuchumi nchini Sudan wamekimbilia mataifa ya jirani, huku ikidaiwa kuwa wenye kipato cha chini ndiyo pekee waliobakia katika mji mkuu wa Khartoum.

**VOA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO LA KAZI IT ANAHITAJIKA

IT ngazi ya certificate au diploma msichana kati ya miaka 20 Hadi 25 kituo Cha kazi chamazi Temeke

**TUPIGIE: 0753 38 28 33**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GREPHSON B. SHOO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 601 BCL – MITSUBISHI FUSO**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Control No. 9910837318186.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**OLIVER RAPHAEL LIMWAGU** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 988 CCH** aina ya **HONLAG.** Chassis namba **LJECJL 63JA016095.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBL/RB/7114/2023.**

## KUPOTELEWA NA VYETI



**NELSON EMMANUEL STANLEY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0631-0129** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **UMOJA SEKONDARI** mwaka 2012. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0112-0672** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **IYUNGA SEKONDARI** mwaka **2015.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/UR/RB/187840/2023**.

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na. 805/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SAID MOHAMED SARWATT**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ALLY SAID SARWATT**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 Mwezi 06 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 01 Mwezi 06 Mwaka 2023.

HAKIMU

TANFIN CONSULTANT

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA/NOTISI

**TANFIN CONSULTANT E.A LTD** Kwa niaba ya **SHREE HINDU MANDAL SACCOS LTD** Tunatoa notisi na Tangazo la mnada kwa Wadaiwa wao wanaosomeka hapa chini wawe wamelipa madeni yao wanayodaiwa na **SACCOS** hiyo kinyume na hapo tutauza dhamana na mali zao kwa njia ya mnada wa hadhara. Mnada utafanyika sehemu dhamana/mali husika ilipo na tarehe kama inavyotangazwa hapo chini

| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | UPENDO KAPOGO/ FRANK MBILINYI | NYUMBA ILIOPO MTAA WA MAVURUNZA, KATA YA KIMARA,MANISPAA YA UBUNGO | 23/06/2023, MUDA: SAA 5: 00 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 2. | OMARY ALLY SALUMU | NYUMBA ILIOPO MTAA WA MJI MPYA, KATA YA BUZA,MANISPAA YA TEMEKE | 5/07/2023, MUDA: SAA 5: 00 ASUBUHI NA KUENDELEA. |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnada utafanyika sehemu dhamana ilipo na zitauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei iliyofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano (75%) italipwa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya mnada. Endapo mteja atashindwa kumalizia 75% ndani ya siku 14 kiasi kilicholipwa awali cha 25% hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
3. Gharama za kubadilisha umiliki **(TRANSFER OF OWNERSHIP)** pamoja na gharama nyingine zinazohusiana na umiliki wa mali hizi ni juu ya mnunuzi.

**Mobile: 0785 944 141, 0699222677**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(MAHAKAMA)**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO ENABOISHU**
**WILAYA YA ARUMERU**
**APPLE PRINT (ABOZER MUSANJEE .......MDAI**
**Dhidi ya**
**META PETRO ..........................MDAIWA**
**HAT I YA KUITWA SHAURINI (SUMMOS GENERAL)**
**(MCA Na. 2/1984)**

**Kwa........................... MEJA PETRO WA KARATU**
Kwa kuwa umelazimika uhudhurie mahakamani ili ujibu shtaka/madai kuwa shahidi kama ifuatavyo
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA TAREHE TAJWA UNAAMRIWA NA JAMHURI** uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya J'NNE tarehe 05/06/2023 saa 3:00 asubuhi au mara baada ya hapo ili shauri hili liweze kusikilizwa.
**USIKOSE KUHUDHURIA**
Fahamu ya kwamba ukikataa kupokea hati hii na kuweka sahihi yako au ukipokea na kuacha kuhudhuria mahakamani ni kosa K/f Na.114 A Sura 16 K/A. Hivyo Mahakama inaweza kukuchukulia hatua kali za kisheria.
**HATI HII IMETOLEWA NA AMRI YANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 18.5.2023**

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU MATHIAS DONALD NDOLOGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye jina la **SAIMON SHEMU MKOBALO** na namba za usajili **T516DDM** aina ya **TOYOTA NOAH** Rangi **NYEUPE**. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/154163/2022**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-11

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Eddy alichanga na kuhudhuria harusi hiyo, na alikuwa mbele kwa kila hatua, akisalimia na kupeana mikono na bwana harusi, akiwa hajui lolote. Alitambuliwa kuwa ni mmoja wa wateja wake kibiashara. Kina Eddy na Maria walipata bahati ya kukutana na kucheza muziki, pale bibi harusi na bwana harusi waliporuhusiwa kucheza muziki kidogo na wahudhuriaji mbalimbali wanaowataka, na wakawa wanaongea kwa sauti ya chini mambo yao bila mtu yeyote kusikia. Mambo hayo yalitokea miaka mitatu iliyopita, lakini leo ameyakumbuka. Akapiga simu ikapokelewa.

"Hallo bibie hujambo?"

"Mhh, leo umekumbuka nini, maana si bure, mvua itanyesha."

"Nimekukumbuka mpenzi wangu wa zamani, nataka nikupe lunch leo."

"Ya kweli hayo, hapana si bure, tena umenipigia kwenye simu ya ofisi, mmh kashehe."

Maria anaifahamu kazi ya Eddy, hivyo simu ile, tena imepigwa ya mezani, alihisi huenda kuna kitu kisicho cha kawaida.

Maria, pamoja na kwamba aliwahi kuwa mpenzi wa Eddy, lakini amekuwa akimsaidia kumpatia taarifa, habari, nyaraka na mambo mbalimbali anayoyahitaji ambayo anajua yanakuwa ni kwa manufaa ya nchi.


"Mimi nikudanganye tena, au unataka nimnyang'anye huyo jamaa urudi tena kwangu?"

"Mhh! Ubavu huyo sasa hivi unao, mwenzako keshafunga ndoa!"

"Basi nitasubiri uzeeke, jamaa atakuacha na kuoa mke mwingine, mimi nipo nitakuchukua tu." Maria alikauka kwa kicheko, halafu akatamka "We Eddy hujaacha tu utundu?"

"Sijaacha na siwezi kuacha, bibi yangu mwenyewe mzaa mama alikuwa hataki hata kukaa na mimi kwa ajili ya utundu, Wajukuu wote anawakusanya na kukaa nao wakati wa likizo, mimi ananikataa anawaambia wazazi wangu simuwezi huyo kaeni naye..."

Kabla hajamaliza, Maria alimkatisha "Bwana ee Eddy mimi niko ofisini hapa, halafu watu wananiangalia, wewe unanichekesha wananishangaa hapa hata wafanyakazi wenzangu, we bwana we, acha kunivunja mbavu, panga siku tuonane, unichekeshe mpaka basi, huu muda wa kazi."




**"Okay nimekuelewa." Alijibu Maria kwa sauti ya chini kidogo, lakini ya msisitizo.**

"Na mimi nipo kazini Maria, na hii simu wala si ya utani, ni ya kikazi, ingekuwa ya utani ningekupigia kwenye simu yako ya mkononi, ninayo hadi leo."

"Enhee unasemaje baba?"

"Ni hivi, naomba nitumie email yako sasa hivi, ili nikutumie jina la mtu ambaye nataka uangalie safari zake hapo Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam."

"Sawa, unachotaka niangalie nini, anavyoondoka, anavyorudi au, au idadi ya safari zake?"

"Nadhani vyote, huyu ni mmoja kati ya wateja wenu wakubwa kusafiri na ndege kwa safari za humu humu ndani, ninachoomba uniorodheshee safari zake za mwezi Novemba hadi katikati ya Desemba, kutoka hapa kuelekea anapoelekea na anaporejea, anatoka hapa anakwenda wapi na siku ambazo ametoka huko na kurejea Dar. Mengine nitakuandikia kwenye email yako, pia ukiniorodheshea, tunaweza kupata kitu kingine cha kuendelea nacho, au kazi nyingine ya kukupa, sawa mpenzi?"

Sauti ya Eddy pamoja na kwamba alijitahidi isibadilike, lakini ilibadilika na kuonekana ya kikazi zaidi na si ya mzaha unaofariji ya mtu na mpenzi wake wa zamani.

"Okay nimekuelewa." Alijibu Maria kwa sauti ya chini kidogo, lakini ya msisitizo.

Tayari Eddy alikuwa anaanza upelelezi wake. Kama kawaida ya upelelezi wake, unaanza eneo ambalo si kila mtu atadhania kuwa anaweza kufanikiwa.

Wakati walioanza wao walianza kwa kukamata waokota makopo na wazoa taka, wakiwahoji wenye nyumba ambao eneo lao kilikutwa kiroba chenye maiti, Eddy alianza na mtu huyu ambaye sasa jina lake analiandika kwenye email ya Maria, mfanyakazi wa Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Julius Nyerere ili amkusanyie data ya safari zake zote anazoondoka Dar na kurejea.

Dhana ni kitu muhimu kwenye upelelezi. Na hasa dhana kwa mtu ambaye si watu wengi anaoamini kuwa anaweza kufanya kilichofanyika.

Na amelipata jina hili baada ya kufanya upembuzi yakinifu na kufahamu kuwa mauaji ya Tess yanaangukia kwenye kundi la nne na la tano la aina ya mauaji na wauaji, akaamua kucheza humo humo.

Maswali ambayo alikuwa akiuliza kwa ujanja ujanja kwa mjomba wa Tessy, ndiyo yaliyosababisha kupata jina la mtu ambaye anadhani anaweza kumsaidia zaidi kwenye kazi yake hiyo. Au kuanza naye upelelezi.

Kwa kawaida, askari mzoefu au mpelelezi anaweza kutaka kukuuliza swali fulani, lakini kwa sababu anajua hutoweza kulijibu kwa hofu au kumlinda mtu fulani, anaweza kufanya ujanja wa kuuliza vitu vingine ambavyo vinafanana na swali lenyewe, halafu likaangukia mle mle alimokuwa akihitaji.

Hakutaka kujisumbua na lolote lile, akili yake ilimtima kuwa akijua ratiba za safari za mtu huyo ndipo anaweza kujua kama anaweza kuwa msaada na kuanza naye upelelezi, au kutafuta kitu kingine, au kubadili aina ya upelelezi kwa ajili ya kusaka muuaji wa mwanamama Tessy.

Aliachana na na kompyuta baada ya kutuma email na sasa hakutaka kujishughulisha na kitu chochote, akanza kusoma magazeti. taarifa moja iliyoandikwa kwenye magazeti matatu tofauti ndiyo iliyomvutia zaidi.

Akakenua meno, na kutojulikana kama ni tabasamu au mshangao. Alirudia tena kusoma sasa mwanzo hadi mwisho. Vichwa vya habari hiyo viliandikwa hivi 'Muuaji wa Tessy bado kizungumkuti.' Lingine likaandikwa 'Polisi wataka uvumilivu mauaji ya Tessy', la tatu liliandikwa 'Bado muuaji anasawa.'

Wakati akisoma habari yenyewe ndani, ilionekana kabisa wananchi wamekata tamaa ya kupatikana kwa muuaji, kwani ni miezi sita sasa inaonekana hakuna chochote kinachoendelea, huku muuaji huyo aliyeua na kukatakata viungo vya marehemu kama nyama ya buchani, akiendelea kula na kunywa uraiani.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# UBAYA, SOMBA KUWANIA UBINGWA WA WBA ASIA

**Na Saada Akida**

BONDIA Mtanzania Abdul Ubaya anatarajia kupanda ulingoni kutetea ubingwa wa dunia wa WBA Asia dhidi ya Ivan Somba kutoka Uganda katika pambano la litakalofanyika kwenye Ukumbi wa The Super Dome Julai 29, mwaka huu jijini, Dar es Salaam. Pambano hilo ambalo limepewa jina la Bongo Fight Championship litahusisha mchezo wa ngumi za kulipwa sambamba na Muay Thai ambao unahusisha kupigana ngumi na mateke.

Akizungumza na Nipashe, mwandaaji wa pambano hilo, Scott Farrell, alisema imekuwa ni ndoto yake ya miaka mingi kuona anasimamia pambano kubwa la kimataifa huku akifanikiwa kuuleta mkanda wa WBC Muay Thai kwa mara ya kwanza hapa Tanzania.

**Farrell alisema pia siku hiyo bondia Em manuel Shija atapanda ulingoni kupimana ubavu na Yusuf Fundi ambao watachuana kuwania ubingwa wa WBC Muay Thai.**

"Kwanza hii ilikuwa ndoto yangu ya miaka mingi kwa sababu tayari nimeshafanya kazi na bondia mkubwa, Manny Pacquiao, lakini katika mataifa tofauti kama Mexico, Afrika Kusini na Tanzania kwa hili jambo la Bongo Fighting Champions ambalo leo (juzi), tunalizindua litakuwa la kipekee sana.

Hii tunatarajia kuifanya kwa mara ya kwanza na matarajio yetu ni kuona linafanyika kwa ukubwa kutokana na sapoti ya kutosha ambayo tumeipata kutoka kwa wadhamini, lakini kwa mara kwanza tumeweza kuleta mkanda WBC Muay Thai, " alisema mratibu huyo.

Naye bondia, Shija alisema amefanya maandalizi mazuri kuelekea pambano hilo kwa sababu anataka kuipa heshima na kuitangaza vyema nchi yake.

Alisema kwa muda ambao amejifua, anaamini hatawaangusha mashabiki wake ambao wanamuunga mkono kila anapokuwa na pambano.

"Naendelea na maandalizi kwa sababu tunaenda kucheza pambano kubwa sana, na ukiangalia huu mchezo tayari ulikuwa umeshawekwa pembeni, nataka kuwaambia nimejiandaa kufanya mambo makubwa ambayo tunaamini tutafikia malengo," alisema Shija.



Wachezaji wa mchezo wa magongo wa Shule ya Sekondari ya Muza, Dar es Salaam wakifanya mazoezi ili kuimarisha viwango vyao kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete Youth Park jijini jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Wasanii Morogoro wapewa neno*

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WASANII wa Morogoro wametakiwa kuhakikisha wanatumia kazi zao kuelimisha jamii namna ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto pamoja na kutoa elimu ya kulinda maadili ikiwamo kukemea ndoa za jinsia moja, imeelezwa.

Agizo hilo limetolewa na Ofisa Michezo na Utamaduni Mkoa wa Morogoro, Grace Njau, wakati akizindua Mtandao wa Maendeleo ya Sanaa na Utamaduni (TAGOSINE) mkoani hapa wenye lengo la kuunganisha washiriki wote wa tasnia hiyo ili kuwa na nguvu ya pamoja.

Njau alisema moja ya faida ya sanaa ni kusaidia nchi katika kuhamasisha na kuleta amani, utulivu na kupiga vita mambo yanayopingana na tamaduni za Kitanzania ikiwamo mapenzi ya jinsia moja na vitendo vya ukatili.

Alisema tangu serikali ya awamu sita kuingia madarakani imekuwa ikithamini tasnia hiyo na kutoa kipaumbele katika mambo mbalimbali yanayochangia maendeleo ya sanaa.

Naye Mwenyekiti wa Taifa wa TAGOSINE, David Msuya, alisema taasisi hiyo inalenga kutangaza miradi yote inayofanywa na serikali ili kutetea taifa kupitia sanaa.

Msuya alisema taasisi hiyo pia imelenga kuendeleza sekta filamu na uigizaji, sanaa na maonyesho, muziki na sanaa ya ufundi ambapo wahusika watasaidiwa kufanya sanaa zao na kutafutiwa masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mwenyekiti wa TAGOSINE mkoani hapa, Abdul-Aziz Salehe, alisema atahakikisha kazi zote za sanaa zinazofanywa Morogoro zinatambulika na kusimamiwa masoko yake wasanii wanufaike na jasho lao.

## Kabbadi yaita 40, Kaole mabingwa

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI 40 wa mchezo wa Kabbadi wanatarajiwa kuunda vikosi vya timu ya taifa ya wanawake na wanaume itakayoingia kambini kujiandaa na mashindano mbalimbali ya kimataifa yatakayofanyika hivi karibuni.

Tanzania inatarajia kupeleka timu katika mashindano ya Kabbadi Afrika yatakayoanza Agosti 21 hadi 29, mwaka huu nchini Cameroon.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Kabaddi Tanzania (TKSA), Michael Chaula, alisema wachezaji hao wamepatikana katika Ligi ya Taifa iliyomalizika hivi karibuni kwenye Uwanja wa Chuo Cha Kampala, Dar es Salaam.

Chaula alisema kikosi hicho kitaingia kambini mapema Julai na Kamati ya Ufundi itafanya mchujo ili kupata nyota wachache watakaokwenda kupeperusha bendera ya nchi katika michuano hiyo.

Wakati huo huo, Kaole wameibuka mabingwa wa Ligi ya Taifa ya Kabbadi kwa wanaume wakati Buffallo ilitwaa kombe hilo kwa upande wa wanawake na St. Joseph wanawake wakishinda tuzo ya nidhamu na KMKM ilichukua kwa upande wa wanaume.

## Expanse Studio kuwajaza washindi

**Na Saada Akida**

MKUU wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Meridianbet Tanzania, Martina Nkurlu, amesema kampuni hiyo imekuja na shindano jipya la 'Expanse Studio', linalompa mchezaji nafasi ya kushinda mgao wa Sh. 500,000.

Nkurlu aliliambia gazeti hili, mashabiki wanatakiwa kucheza mchezo huo mpya unaosimamiwa na 'wakali' wa Kasino ya mtandaoni wenye sloti rahisi kushinda kama aviator, poker na roullete, huku wakijipanga kugawa 'mpunga' wa kutosha kwa washindi kwa mwezi huu.

Alisema michezo ya sloti inayohusika kutoa mtonyo huu ni Book of Egypt, Bounty hunters, Capital City Derby, Forest Rock, Pirates Power, Spinning Buddha, Book of Eskimo, Wild icy fruits, Mayas Treasure, Wild White Whale na Planet Power.

"Kipindi chote cha shundano wachezaji watashinda kulingana na idadi ya mizunguko inayochezwa katika michezo ya watoa huduma ya Expanse kutoka kasino ya mtandaoni ya Meridianbet ambayo orodha ya nafasi ndani ya mchezo inaonekana saa 24 baada ya mwisho wa mashindano," alisema Nkurlu.

Alisema kulingana na orodha ya mwisho kwa nafasi, wachezaji watano walioshika nafasi za juu watatunukiwa bonasi ya kasino ya mtandaoni katika viwango vitano.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MESSI AITWA MAREKANI

INTER Miami imempa, Lionel Messi (35), ofa ya euro 50 kwa mwaka ili kuitumikia klabu hiyo ya Ligi Kuu Marekani (MLS), kwa miaka minne baada ya mshambuliaji huyo wa Argentina kuthibitika anAondoka Paris St-Germain msimu huu. (*Sport*)

### BENZEMA AMFUATA RONALDO

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Karim Benzema, mwenye umri wa miaka 35, atajiunga na klabu ya Saudi Arabia Al-Ittihad mara mkataba wake wa Real Madrid utakapokamilika mwezi huu. (*ESPN*)

### MODRIC KWENDA SAUDIA

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Croatia, Luka Modric, mwenye umri wa miaka 37 ameiambia Real Madrid anatarajia kuikubali ofa ya euro 120 ili kucheza Saudi Arabia kwa misimu mitatu ijayo. (*Okdiariovia Sport*)

### OSIMHEN ANUKIA UNITED

KLABU ya Newcastle United inajiandaa kupambana na Manchester United kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 24 akitokea Napoli. (*Gazzetta dello Sport via Mirror*)

### RICE : NITABAKI ENGLAND

KIUNGO wa kati wa West Ham ya England, Declan Rice, angependelea kubakia kwenye Ligi Kuu England msimu huu wa joto anapojiandaa kukataa kuhamia Bayern Munich, huku Arsenal na Manchester United zikimtaka zaidi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. (*Mail*)

### KOVACIC KUTUA CITY

KLABU ya Manchester City inakaribia kukamilisha usajili wa kiungo wa kati wa Croatia, Mateo Kovacic, mwenye umri wa miaka 29 kutoka Chelsea. (*Football Insider*)

### SPURS YAPATA KOCHA

BOSI wa Celtic, raia wa Australia, Ange Postecoglou, anaweza kuthibitishwa kuwa kocha mpya wa Tottenham Hotspur mapema wiki ijayo. (*Sun*)

### ALLARDYCE KUTEMWA LEEDS

KOCHA, Sam Allardyce, mwenye umri wa miaka 68 hatapewa mkataba mpya wa kubakia Leeds United baada ya kushindwa kufanya vyema katika mechi zake nne alizopewa za mwisho mwa ligi ili kuinusuru timu hiyo isishuke daraja. (*Telegraph*)

### CANCELO KUBAKIA BAYERN

JOAO Cancelo wa Manchester City ana uwezekano mkubwa wa kufanya uhamisho wake wa mkopo kwenda Bayern Munich kuwa wa kudumu msimu huu wa joto. Beki huyo wa pembeni wa Ureno mwenye umri wa miaka 29 hataki kurejea England (*Abendzeitung*)

### CHELSEA YAIBANIA BRIGHTON

KLABU ya Chelsea imekataa dau la pauni milioni 30 kutoka kwa Brighton kwa ajili ya kumnunua beki, Levi Colwill, mwenye umri wa miaka 20. (Mail)

### CHALOBAN ATAJWA MILAN

INTER Milan inapambana kumsajili beki wa kati wa Chelsea, Trevoh Chalobah, mwenye umri wa miaka 23. (*Standard*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND: NITAPAMBANA TUSHINDE MATAJI MATATU

**MANCHESTER,** England

●●● Mshambuliaji huyo akiri wana kibarua kigumu katika fainali hizo ambazo...

MANCHESTER City ambao wameshinda ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu, wanaweza kuongeza taji lingine kama wataifunga Manchester United katika mechi ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Inter Milan itakayochezwa leo na watakapoikabili Inter Milan kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hapo Juni 10, mwaka huu.

**United ilishinda mataji hayo matatu mwaka 1999 na ndio timu pekee ku toka i England kushinda mataji matatu kwa msimu mmoja.**

Na Erling Haaland amesema litakuwa jambo la kihistoria wao kutwaa mataji hayo matatu msimu huu.

"Itakuwa historia ya kweli na tunatakiwa kuifikia," alisema Haaland ambaye ana umri wa miaka 22.

Licha ya kutawala ligi ya nyumbani, City bado hawajawahi kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Haaland ana matumaini huu ndio wakati wa kuonyesha ubora wao kwenye mashindano makubwa ya Ulaya.

"Hii ndio sababu walininunua mimi, kupata hili, hatuwezi kuficha hilo," alisema Haaland akimwambia Mhariri wa BBC Sports, Dan Roan.

"Itamaanisha kila kitu. Nitafanya kila ninawezalo kujaribu na kuhakikisha hili jambo linatokea. Ni ndoto yangu kubwa na nina matumaini itakuwa kweli."

Aliongeza: "Lakini halitakuwa jambo rahisi - ni fainali mbili dhidi ya timu nzuri ambazo zitafanya kila ziwezalo kuhakikisha zinatumaliza.

"Watakuwa na hamasa kubwa, watakuwa tayari na tunatakiwa kucheza kwa kiwango chetu cha juu kabisa, kwa sababu tukicheza kwa ubora wetu, tutakuwa na nafasi kubwa ya kufikia mafanikio hayo."

City waliwapiku Arsenal msimu huu na kutwaa taji lao la tatu mfululizo la Ligi Kuu England chini ya Kocha, Pep Guardiola.

## Messi leo kucheza Mechi mwisho PSG

**PARIS,** Ufaransa

LIONEL Messi sasa ni rasmi ataondoka Paris Saint-Germain baada ya miaka miwili ya kukaa klabuni hapo, Kocha Mkuu, Christophe Galtier, alisema jana.

ESPN iliripoti mwezi uliopita Messi ataondoka PSG wakati mkataba wake utakapokamilika kipindi cha majira ya joto, huku akiwa anawaniwa na klabu ya Saudi Arabia ya Al Hilal, ambayo ni wapinzani wa timu anayoichezea Cristiano Ronaldo, Al Nassr.

Na Galter aliwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa mwisho wa PSG wa Ligi Kuu Ufaransa dhidi ya Clermont Foot leo kuwa: "Najisikia fahari kumnoa mchezaji bora kwenye historia ya soka.

"Hii itakuwa mechi yake ya mwisho kwenye dimba la Parc des Princes, na natumaini ataagwa kwa shangwe kubwa.

"Mwaka huu amekuwa mchezaji muhimu sana kwa timu yetu. Hakuwahi kuzungumza lolote baya kwa timu.

"Mara zote alikuwa tayari kwa timu. Ulikuwa wakati bora zaidi kufanya naye kazi kwa kipindi chote alichokaa hapa."


Messi alichangia mabao 21 na asisti 20 kwa PSG kwenye mashindano yote msimu huu.

Messi alijiunga na mabingwa hao wa Ufaransa mwaka 2021 baada ya kukaa Barcelona miaka 21.

Pamoja na Kylian Mbappe and Neymar, alisaidia PSG kushinda taji la Ligue 1 katika msimu yote miwili aliyokaa kwenye mji mkuu huo wa Ufaransa.

Hata hivyo, kutulewa mfululizo kwenye hatua ya 16 kwenye Ligi ya mabingwa, kuna maanisha kwamba, klabu hiyo bado inalisaka taji lake la kwanza la Ulaya.

Alifunga mabao 32 katika mechi 74 kwenye mashindano yote kwa PSG, pamoja na asisiti 35.



# BENZEMA KUONDOKA REAL MADRID




**MADRID,** Hispania

KARIM Benzema ataondoka Real Madrid mkataba wake utakapomalizika mwezi huu na kujiunga na Al Ittihad ya Saudi Arabia, vyanzo vimeiambia ESPN.

ESPN iliripoti mapema wiki hii Benzema alipewa mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya Euro milioni 400 kuhamia Saudi Arabia Januari, mkataba sawa na wa Cristiano Ronaldo, aliyejiunga na Al Nassr baada ya kuondoka Manchester United.

Benzema mwenye umri wa miaka 35 amekaa kwa misimu 14 Bernabeu, na kuwa mfungaji bora wa pili wa wakati wote wa klabu hiyo na kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tano, mataji manne ya LaLiga na Ballon d'Or moja.

Mshambuliaji huyo wa kati alitarajiwa kusalia Madrid kwa msimu mmoja zaidi hadi Juni, 2024 lakini amechagua kutafuta changamoto mpya.

Benzema alikataa kuhusishwa na ripoti hizo siku ya Alhamisi alipopokea tuzo ya gwiji wa Marca.

"Kwa nini ninahitaji kuzungumzia mustakabali wangu? Niko Real Madrid. Sio kila kitu unachosoma kwenye mtandao ni ukweli," alisema.

Nahodha huyo wa klabu ya Madrid amekuwa na msimu wa majeruhi -- alikosa Kombe la Dunia la 2022 nchini Qatar kwa tatizo la misuli ya paja -- lakini bado alifunga mabao 18 katika mechi 23 za LaLiga, pamoja na mabao manne katika hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Benzema alijiunga na Madrid akitokea Lyon mwaka 2009 kama mmoja wa washambuliaji chipukizi.

# Ronaldo kubakia Saudi Arabia

**RIYADH, Saudi** Arabia

CRISTIANO Ronaldo amethibitisha atabakia Saudi Arabia katika Klabu ya Al Nassr msimu ujao, huku akisema Ligi ya Saudi Pro League (SPL) inahitaji kuimarika ili iwe moja ya ligi kubwa duniani.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 38 alifunga mabao 14 katika michezo 16 ya Al Nassr yenye maskani yake Riyadh kufuatia uhamisho wake wa Januari baada ya kuvunjwa kwa mkataba wake na Manchester United kwa makubaliano hapo Novemba, mwaka jana.

Lakini licha kufurahia maisha yake mafupi Saudi Arabia, Ronaldo amesema maeneo kama vile maamuzi ya teknolojia ya VAR yanahitaji kuboreshwa.

"Ligi ni nzuri sana," alisema Ronaldo katika mahojiano na SPL.

"Lakini nadhani tuna nafasi nyingi sana za kukua, ligi ina ushindani, tuna timu nzuri sana, wachezaji wazuri sana wa Kiarabu, lakini wanahitaji kuboresha zaidi miundombinu.

"Hata waamuzi, mfumo wa VAR, uwe wa haraka zaidi, nadhani mambo mengine madogo wanatakiwa kuyaboresha.

"Lakini nina furaha hapa, nataka kuendelea hapa, nitaendelea hapa. Na kwa maoni yangu wakiendelea kufanya kazi wanayotaka kuifanya hapa, kwa miaka mitano ijayo, nadhani ligi ya Saudia inaweza kuwa moja ya ligi tano bora duniani."

"Kama wanakuja wachezaji wakubwa na wenye majina makubwa, wachezaji chipukizi, 'wachezaji wazee,' wanakaribishwa sana kwani hilo likitokea, ligi itaimarika kidogo," alisema.

Ronaldo amemaliza msimu wake wa kwanza katika klabu ya Al Nassr bila taji lolote kutokana na Al Ittihad kutwaa taji la SPL na wapinzani wao Al Hilal wakinyanyua Kombe la Mfalme.

Na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno amekiri kwamba alitarajia kushinda baadhi ya mataji msimu huu kufuatia kuhamia kwake Al Nassr.



## HABARI MICHEZO

# WACHEZAJI YANGA PRINCESS WALALAMIKA KUTELEKEZWA

Na Saada Akida

WACHEZAJI wa Yanga Princess inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania wamegoma kuondoka kambini kutokana na kushinikiza kulipwa madai yao, imefahamika.

Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu wa 2022/2023 ilimalizika tangu Mei 17, mwaka huu kwa Maafande wa JKT Queens kutwaa ubingwa, ikicheza mechi 18 bila kupoteza. Tayari wachezaji wa timu nyingine wameshavunja kambi na kwenda kwenye mapumziko, wakisubiri kuitwa hapo baadaye kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya.

**Taarifa zilizopatikana jijini zinasema wachezaji wote wazawa na wageni wameendelea kubakia katika nyumba wali yokuwa wanaishi ili yopo Mikocheni wakisubiri malipo yao.**

"Wachezaji wanadai malimbikizo ya mishahara na fedha za usajili, wamesema hawaondoki, wanawasubiri viongozi warejee nchini," kilisema chanzo chetu.

Chanzo hicho kilisema viongozi wamewakatia tiketi wachezaji wa kigeni za kuondoka nchini Juni 8, mwaka huu lakini wameahidi hawataondoka bila ya kulipwa madai yao.

"Inasikitisha, yaani tangu tumemaliza ligi hakuna kiongozi ambaye alikuja kambini kuwatembelea au kuwapa mwongozo wa klabu baada ya kumaliza msimu 2022/23," kiliongeza chanzo hicho.

Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Fred Mbuna, aliliambia gazeti hili tayari ameshakabidhi ripoti na taarifa za wachezaji kugoma kuondoka naye ameziona mtandaoni.

Mbuna alisema wachezaji wanatakiwa kuvumilia kwa sababu kwa sasa viongozi wakuu wote wako Algeria kwa ajili ya mechi ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika inayochezwa leo dhidi ya wenyeji USM Alger.



Beki wa Simba, Henock Inonga (kulia), akiwania mpira katika mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa kuwakaribisha Polisi Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa Jumanne. **PICHA: SIMBA SC**

# Yanga: Tumefuata kombe

INATOKA UK 24

alisema: "Nataka kuwaambia tuko tayari, hatujakata tamaa, tunaenda kutafuta ushindi."

Takwimu zinaonyesha Yanga imeshinda mechi nne za ugenini katika michuano hiyo kati ya mechi sita ilizocheza tangu michezo ya mchujo.

Ilishinda bao 1-0 dhidi ya Club Africain ya Tunisia na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Rivers United mabao 2-0 na dhidi ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini walishinda magoli 2-1.

Pia takwimu zinaonyesha USM Alger haijapoteza mechi yoyote kwenye uwanja wake wa nyumbani tangu kuanza kwa michuano hiyo, ikiwa imeruhusu bao moja tu, ilipocheza dhidi ya Al Akdar na mchezo huo ulimalizika kwa wenyeji kushinda mabao 4-1.

USM Alger pia haijashinda mechi yoyote ya ugenini kabla ya kucheza mchezo wa kwanza wa fainali dhidi ya Yanga, ikiwa imetoa sare na kupoteza michezo miwili, dhidi ya Marumo Gallats ilipofungwa mabao 2-0 na walipovaana na ASFAR ya Morocco walifungwa magoli 3-2.

Kikubwa zaidi kwenye mechi ya leo ni uwezekano mkubwa wa Mayele, kukabidhiwa tuzo ya ufungaji bora wa michuano hiyo, akiwa amepachika mabao saba mpaka sasa, Mkongomani huyo anafuatiwa na mshambuliaji wa Marumo Gallants, Ranga Chivaviro, ambaye amefunga magoli sita, lakini timu yake ikiwa imeshatolewa.

Wachezaji anaoshindana nao kwa sasa Khaled Bousseliou, mwenye mabao manne na Zinneddine Belaid aliyefunga magoli mabao matatu, wote wanaichezea USM Alger.

## Klabu 18 kuchuana Ligi ya Wanawake

Na Abdallah Mataka

JUMLA ya timu 18 zimethibitisha kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa wa Mikoa ya Wanawake mwaka huu (WRCL 2023), yatakayofanyika hivi karibuni, imeelezwa.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alizitaja timu hizo zilizothibitisha kushiriki ligi hiyo ni Mabibo Queens, Sayari Queens na Young Star Queens zote kutoka Dar es Salaam, Mara Princess (Mara), Gets Program (Dodoma), Mwanga City Queens (Kigoma) na Coastal Ladies ya jijini Tanga.

Ndimbo alizitaja nyingine ni Raha Queens (Simiyu), Shadow Girls (Geita), Mandozi Queens (Mwanza), Maendeleo Queens (Songwe), Itwelele Queens (Rukwa), Ilula FDC Queens (Iringa), Chipuputa Queens (Mtwara), Mpaju Queens (Mbeya), Ifakara Home Queens (Morogoro), Emayan Queens (Arusha) na Ziba (Tanga).

"Ikumbukwe dirisha la kuthibitisha ushiriki wa ligi hii limefungwa tangu Mei 30, 2023," Ndimbo alisema.

Ligi hiyo itatoa timu mbili zitakazopanda daraja kucheza Ligi Daraja la Kwanza ya Wanawake kwa msimu ujao wa 2023/2024.

## Simba SC yafunguka itamaliza maumivu

INATOKA UK 24

kumaliza msimu kwa kuwapa furaha mashabiki wao kwa kushinda mechi hizo mbili.

Kajula alisema watafanya kazi kubwa kwenye maboresho ya kikosi kwa kuwaongeza wachezaji wazuri ambao watatoka katika klabu zilizofanya vizuri katika michuano ya kimataifa.

"Tumekutana na kocha wetu Robertinho ambaye ameweka mezani mapendekezo yake ya awali ya usajili kabla ya kutukabidhi ripoti ya msimu baada ya ligi kufikia tamati.

Tunatambua haukuwa msimu mzuri kwetu, tunajua tulipojikwaa na tunachokifanya kwa sasa ni kuangalia pale tulipokwama, kuboresha kwa ajili ya kupata matokeo chanya katika mashindano tutakayoshiriki msimu ujao," alisema mtendaji huyo.

Aliongeza mapungufu yote yaliyotokea msimu huu yanafanyiwa kazi kwa sababu wanafahamu katika mpira unatakiwa kujiimarisha ili urejee ukiwa imara na tayari kupata matokeo chanya.

# Michezo

Nipashe

Jumamosi Juni 3, 2023





Benzema kuondoka Real Madrid

UK. 22




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana (kulia aliyesimama), akiwatakia heri na ushindi wachezaji wa Yanga kuelekea mechi ya mkondo wa pili ya fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji USM Alger itakayochezwa leo nchini Algeria. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simba SC yafunguka itamaliza maumivu

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikikabiliwa na michezo miwili ya kukamilisha msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa klabu hiyo wamebainisha watafanya mapinduzi yakayosaidia timu yao kutimiza malengo yake katika msimu mpya wa mwaka 2023/2024.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba iko kwenye nafasi ya pili ikiwa na pointi 67 huku watani zao, Yanga wenye pointi 74 kibindoni wameshatangazwa mabingwa wapya wa msimu huu, kila timu ikibakisha mechi mbili kumaliza msimu.

Kikosi cha Mnyama sasa kinaendelea na mazoezi kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena chini ya Kocha Mkuu Robert Oliveira 'Robertinho' kwa ajili ya mchezo unaofuata dhidi ya Polisi Tanzania utakaopigwa Jumanne na baadaye itafunga pazia kwa kuwakaribisha Coastal Union Juni 9, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema wakati klabu inajipanga kuhakikisha wanaimarisha kikosi lakini pia wanahitaji

INAENDELEA UK 23

# Yanga: Tumefuata kombe

## ●●● Kocha, wachezaji waahidi kuweka historia, hawana presha kama...

**Na Adam Fungamwango**

FAINALI ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika inakamilika kwa wenyeji USM Alger kuwakaribisha mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga katika mechi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Juillet wa Tano ulioko jijini Algiers nchini Algeria.

**Ni mechi ya mkondo wa pili ita kayoanza saa 4:00 usiku kwa saa za Tanzania baada ya mchezo wa kwanza uliochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, kumalizika kwa Yanga ikilala mabao 2-1.**

Wawakilishi hao wana kazi moja tu ya kushinda mechi hiyo kuanzia mabao 2-0 ili kutwaa kombe hilo na kulileta kwenye ardhi ya Tanzania kwa mara ya kwanza.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema anadhani wachezaji wake hawatacheza tena kama walivyocheza katika mechi ya kwanza iliyochezwa hapa nchini, na badala yake watakuwa wameshaondoa presha ya fainali.

Nabi alisema ametengeneza mkakati na mfumo ambao watautumia kucheza ugenini ili uwape matokeo mazuri.

Kocha huyo raia wa Tunisia alisema mechi hiyo itakuwa ngumu kama wachezaji wake hawatabadilika na wakifuata maelekezo yake, mambo yatakuwa mazuri.



"Pamoja na tulimkosa mchezaji kama Khalid Aucho, lakini pia ilikuwa ni presha ya fainali, wachezaji wangu wakicheza kama ilivyokuwa Dar es Salaam mechi itakuwa ngumu kwetu, lakini wakibadilika kama walivyoniahidi na mpango mkakati niliyoutengeneza matokeo yanaweza kuwa mazuri upande wetu, ila niseme tu mechi itakuwa ngumu kwa sababu mbili, USMA ni wazuri na pia hii ni fainali, tena ya mwisho," alisema Nabi.

Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema kila kitu kimeenda sawa kuhusiana na maandalizi ya mchezo huo na sasa wanasubiri muda ufike ili wachezaji wakatimize majukumu kama walivyoelekezwa na walimu wao.

"Tunaamini kuna kitu tunaweza tukakifanya na tukabadilisha matokeo mabaya tuliyoyapata kwenye mchezo wa kwanza, kila mtu yuko makini na mchezo huu hasa wachezaji na benchi la ufundi ambalo baada ya kuona mapungufu kwenye mechi ya kwanza wameyafanyia kazi, tunachosubiri ni muda tu wa kuanza pambano," alisema Walter.

Straika tegemeo wa Yanga, Fiston Mayele, alisema anaamini Yanga inauwezo wa kushinda mechi ya leo na kuandika rekodi mpya kwa Watanzania.

Mayele alisema kila mchezaji wa Yanga ameahidi kuonyesha kiwango cha juu ili kutimiza ndoto yao ya kubeba ubingwa wa michuano hiyo na kutimiza malengo yao kwa msimu huu.

"Tumeshasahau mechi iliyopita, sisi wachezaji hatujataka tamaa, ile siku tukiamka vizuri na mimi mwenyewe nikiamka vizuri, nitaamua matokeo, tumejipanga kucheza katika kiwango cha juu, kama tutatulia, ninaamini tutashinda na kurudi Tanzania na kikombe, hakika tumejipanga," Mayele alisema.

Winga machachari, Bernad Morrison

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >